**MADA:**

# ATHARI ZA SHENG' KWA KISWAHILI MIONGONI MWA WATACHONI WAISHIO LWANDETI.

**NA:**

**REHEMA MERCY MAKOKHA**

**NAMBARI YA USAJILI: C50/89950/2016**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa popote kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile kingine.

Rehema Mercy Makokha.

(Mtahiniwa)

Sahihi............ Tarehe....11....2....22

Wasimamizi

Dkt. Ayub Mukhwana

Sahihi.............................. Tarehe....11/2/2022

Prof. Iribe Mwangi.

Sahihi.............................. Tarehe....11/02/2022......

## TABARUKU

Kazi hii ya uzamili naitabarukia wazazi wangu wapendwa Makokha Ezero na Catherine Nasambu kwa kunielimisha na kunifunza jinsi ya kukabiliana na changamoto za maisha. Pia, ndugu na dada zangu, mume na watoto wangu wapendwa Lucky na Prudence kwa mawaidha yao na uvumilivu wao kwangu nilipokuwa katika harakati za utafiti na pia wanafunzi wangu ambao walifanikisha katika kupata data ya utafiti huu. Nyote ni zawadi kubwa kwangu kutoka mbinguni. Nawaombea Baraka tele za Mwenyezi Mungu kwa kunipa wakati wa utulivu katika kipindi chote cha utafiti.

## SHUKRANI

Nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa kila mmoja ambaye alichangia kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha utafiti huu. Namshukuru Mungu kuniongoza kwa vyovyote vile na kunipa afya. Pia, nawashukuru wahadhiri wangu wote kwa maarifa ambayo walinipa wakiwemo Prof. Habwe, Mwalimu Sanja, Dkt. Jerono, Prof. Mbuthia, Prof. Kineene, Prof. Mbatia, na Dkt. Jefwa. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimazi wangu waliojitolea kwa vyovyote vile kuhakikisha kuwa wamenielekeza ipasavyo na ambao ni Prof. Iribe Mwangi na Dkt. Ayub Mukhwana. Nawashukuru pia wanafunzi wenzangu ambao ni Ruth, Mbukha, Beatrice, Agnes, Dan,Yego, Anne, Chirchir, Lucy, Robert, Nyageteria, Njomo, Njoro, Jacinta, Nicodemus, Violet, Dickens, Dorcas, Gladys, Ogelo, Irine, na Thomas ambao tulishirikiana bega kwa bega kuhakikisha kwamba tumeindeleza safari hii ya Shahada ya Uzamili pamoja. Familia yangu pia nawaombea mbarikiwe sana kwa uvumilivu na uelewa wenu wakati nilikuwa katika harakati za masomo yangu. Ahsanteni sana nyote.

## IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia utafiti kuhusu athari za lugha kipindi ya Sheng' miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili ambao ni wazaliwa Watachoni na wanaotoka katika lokesheni ya Lwandeti. Tumetalii vyanzo vya utumizi wa lugha hii ya Sheng' kwa kuangalia ni kwa namna gani leksimu za Sheng' huundwa na ni kwa kiwango gani lugha hii imeathiri lugha sanifu ya Kiswahili haswa katika kitengo cha kimofolojia na kile cha kisemantiki. Pia tumeangalia ni kwa namna gani makosa haya yatokanayo na Sheng' huathiri wanafunzi katika shule za upili ambazo ni pamoja na shule ya upili ya Lukhokho, shule ya upili ya Lwandeti D.E.B na shule ya upili ya Maturu katika kiwango cha mitihani ambayo ni ya kitaifa. Tumetumia mifano ya Insha ambazo wanafunzi hawa wameziandika kisha kuonyesha makosa ambayo wamefanya kwa kupigia mistari makosa hayo na kisha kuonyesha majibu sahihi juu yake kwa kutumia kalamu ya wino mwekundu. Pia, tumehoji walimu wanaolifunza somo hili la Kiswahili na kutambua jinsi lugha hii huenea katika mazingira ya shuleni. Vijana wengi haswa wa mijini wanatumia lugha hii ya Sheng' katika mawasiliano yao hivyo utafiti huu umeonyesha kwamba siyo tu vijana wa mijini wanaoitumia lugha hii bali pia imeenea vijijini na kutumika na vijana wote katika mawasiliano yao. Tumependekeza tafiti zaidi zifanywe kuhusiana na suala hili nyeti ili kuepusha athari hasi kama hizi sio tu miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili walio Watachoni bali wakenya kwa jumla.

**YALIYOMO**

**UNGAMO…** ........................................................................................................ ii

**TABARUKU** ........................................................................................................ iii

**SHUKRANI** ........................................................................................................ iv

**IKISIRI** ........................................................................................................ v

**Maelezo Ya Dhana Zilizotumiwa Katika Utafiti** ........................................................ x

**SURA YA KWANZA**

**1.1 USULI WA MADA…** ........................................................................ 1

**1.2 TATIZO LA UTAFITI** ........................................................................ 2

**1.3 MASWALI YA UTAFITI** ........................................................................ 3

**1.4 MALENGO YA UTAFITI** ........................................................................ 3

**1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA…** ............................................................ 3

**1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI** ............................................................ 4

**1.7 MSINGI WA KINADHARIA…** ............................................................ 5

**1.7.1 Nadharia ya Lugha Kadirifu** ............................................................ 5

**1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA…** ............................................................ 7

**1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu Athari za Sheng' kwa Lugha ya Kiswahili** .................. 9

**1.9 MBINU ZA UTAFITI** ............................................................ 10

**1.9.1 Mbinu za Kukusanya Data…** ............................................................ 11

**1.9.2 Vifaa vya Utafiti** ............................................................ 11

**1.9.3 Mbinu za Kuchanganua na Kuwasilisha Data…** .......................................... 12

**1.9.4 Maadili katika Utafiti** ............................................................ 12

**1.10 HITIMISHO** ............................................................ 13

**SURA YA PILI**

**2.0 MBINU ZINAZOTUMIKA KATIKA KUUNDA LEKSIMU ZA SHENG'.**

**2.1 Utangulizi** ............................................................ 14

**2.2 MBINU ZA KUUNDA LEKSIMU ZA SHENG'** ........................................ 14

**2.2.1 Uambishaji** .......... **14**

**2.2.2 Ukatizaji** .......... **15**

**2.2.3 Unyambulishaji** .......... **16**

**2.2.4 Onomatopia** .......... **18**

**2.2.5 Upolisemia** .......... **19**

**2.2.6 Ubunaji** .......... **19**

**2.2.7 Akronimu** .......... **20**

**2.2.8 Uhulutishaji** .......... **21**

**2.2.9 Uambatishaji** .......... **21**

**2.2.10 Ubadilishaji silabi** .......... **22**

**2.2.11 Ukopaji** .......... **23**

**2.2.11.1 Ukopaji Utohozi** .......... **23**

**2.3 HITIMISHO** .......... **24**

**SURA YA TATU**

**3.0. MAHUSIANO YA FAHIWA KATIKA SHENG'**

**3.1 Utangulizi** .......... **25**

**3.2 Sinonimia** .......... **26**

**3.3 Haiponimia** .......... **27**

**3.4 Kapitonimu** .......... **28**

**3.5 Polisemia** .......... **28**

**3.6 Antonimia…** .......... **29**

**3.7 HITIMISHO** .......... **30**

**SURA YA NNE**

**4.0 MAKOSA KATIKA KAZI ZA WANAFUNZI.**

**4.1 Utangulizi........................................................................................ 31**

**4.2 Makosa ya Kimofolojia.................................................................... 31**

**4.2.1 Ukopaji.......................................................................................... 31**

**4.2.2 Ubunaji..........................................................................................32**

**4.2.3 Uambishaji..................................................................................... 33**

**4.2.4 Upolisemia ....................................................................................33**

**4.3 Makosa ya Kisemantiki .....................................................................35**

**4.4 Mikakati ya Kuzuia Makosa Yatokanayo na Sheng' ................................37**

**4.5 HITIMISHO........................................................................................ 39**

**SURA YA TANO**

**5.0 MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO.**

**5.1 Muhtasari...........................................................................................41**

**5.2 Mahitimisho........................................................................................ 43**

**5.3 Mapendekezo...................................................................................... 44**

**MAREJELEO ..........................................................................................45**

**KIAMBATISHO A. (MAHOJIANO) ..........................................................xii**

**KIAMBATISHO B. (VIELELEZO VYA INSHA)........................................... xiv**

**Maelezo ya Dhana Ambazo Zimetumiwa Katika Utafiti.**

**Lugha ya kwanza** - Ni lugha ambayo mtu yeyote yule hutangulia kujifunza haswa mtoto anapozaliwa.

**Lugha ya pili** - Hii ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza.

**Msimbo** - Ni njia ambazo watu huwasiliana nazo hasa kupitia ishara na nambari ili kuwasilisha ujumbe fulani.

**Lugha kadirifu** - Hii ni lugha ambayo huwa kati ya lugha ya matumizi ya lugha ngeni na ile ya asili.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 USULI WA MADA.

Katika nchi ya Kenya, Sheng' ni lugha msimu ya Kiswahili ambayo ni maarufu haswa miongoni mwa vijana. Katika hali halisi ni vijana wanaojifunza kwa uzuri zaidi lugha ya pili au hata ya tatu. Lugha msimu ya Sheng' ilipoanza iliambatanishwa haswa na vijana wa mijini na haswa mji wa Nairobi lakini kwa sasa inatumiwa na Wakenya kwa ujumla wao hadi katika viwango vya vijijini. Utafiti huu wetu unahusu athari za lugha msimu ya Sheng' katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu inayotahiniwa katika shule za upili miongoni mwa wanafunzi Watachoni katika lokesheni ya Lwandeti ambayo kimsingi hupatikana katika mazingira ya vijijini katika kaunti ya Kakamega.

Watafiti wa awali wana mawazo kuwa lugha ya Sheng' huvuka mipaka katika matumizi yake na ni jambo ambalo limetufanya sisi kama watafiti tujiulize nafasi ya lugha hii kipindi katika suala zima la ufundishwaji wa Kiswahili ni lipi? Hii ni kwa kuwa lugha ya Sheng' na ambayo ilichukuliwa hapo awali kuwa ya mijini kwa sasa lugha hii imevuka mipaka yake na inatumika sasa hata katika vijiji. Katika muktadha wa utafiti huu wetu, vijiji ambavyo tumeegemea katika utafiti wetu ni vile ambavyo vinapatikana katika lokesheni ya Lwandeti na ambavyo wenyeji wake wengi ni wazungumzaji wa lahaja ya Kibaluhya iliyo ya Kitachoni.

Tumeweza kutofautisha wale Watachoni wanaozungumza lugha ya Sheng' kwa kuangazia wale wapatikanao katika kaunti ya Bungoma na wale wa kaunti ya Kakamega. Hii ni kwa sababu Watachoni wapatikanao katika kaunti ya Bungoma wanaishi ama mjini Webuye au kando kando ya mji huu. Hali hii ni tofauti na ya Watachoni waishio katika kaunti ya Kakamega ambao makazi yao ni ya vijijini na ni kwa misingi hii ambapo tumechagua kushughulikia lokesheni ya Lwandeti huku tukiangazia suala zima la ufundiswaji wa Kiswahili sanifu kutokana na athari za lugha kipindi ya Sheng' katika vijiji.

Utafiti huu wetu ambao unahusu athari za lugha kipindi ya Sheng' katika ufundishwaji wa lugha ya Kiswahili sanifu katika shule za upili katika lokesheni ya Lwandeti katika kaunti ya Kakamega. Kimsingi, lugha ya Kiswahili na ambayo ni lugha rasmi na pia lugha ya taifa nchini Kenya, ni lingua franka ambayo umuhimu wake katika elimu na maendeleo katika ujumla wake nchini Kenya hauwezi kupuuzwa au kuchukuliwa kijuujuu ikizingatiwa kuwa

lugha hii ya Sheng’ na ambayo ni lugha kipindi ya Kiswahili ina umaarufu sana na hutumika haswa katika nyanja nyingi katika jamii. Mfano, ni katika matangazo ya kisiasa na hata pia katika matangazo ya kibiashara. Hivyo, tumeonelea kuwa ni muhimu kutafiti ili tubaini athari za lugha hii msimu ya Sheng’ katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wakenya wote kukiwemo hata wale ambao wanaishi katika vijiji.

Mwishoni mwa utafuti wetu tumebainisha matokeo ambayo yanaakisi athari za hii lugha kipindi ya Sheng’ katika ufundishwaji wa Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi waishio vijijini nchini Kenya.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI.

Tafiti za Kachipela (2014) na Mekonge (2016) zilibaini kuwa kazi nyingi za Kiswahili ambazo ziliandikwa na wanafunzi wa shule za upili huwa na makosa mengi ambayo bila shaka husababisha matokeo mabaya katika mitihani yao ya kitaifa katika somo la Kiswahili. Utafiti wa Kachipela ulijikita katika mazingira ya jiji la Nairobi nao wa Mekonge ulijikita katika mji wa Kisii. Utafiti wetu huu umekusudia kuchunguza na kutathmini iwapo lugha kipindi ya Sheng’ husababisha makosa ya kimofolojia na ya kisemantiki katika kazi za Kiswahili ambazo zimeandikwa na wanafunzi katika shule za upili miongoni mwa Watachoni katika lokesheni ya Lwandeti na ambayo ni mazingira ya vijijini. Sisi kama watafiti tumechunguza makosa yanayojitokeza katika sarufi ya Kiswahili kwa kurejelea vipengele vya mofolojia na semantiki na yaliyotokana na athari za Sheng’ katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu kinachokubalika katika mazingira ya shuleni na hasa kwa ajili ya mitihani. Suala la athari za Sheng’ katika lugha ya Kiswahili limetafitiwa na wataalamu wengi sana lakini katika udurusu wetu maktabani hatukupata tafiti zozote zilizoshughulikia athari za Sheng’ katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili miongoni mwa Watachoni waishio katika kijiji cha Lwandeti katika kaunti ya Kakamega. Kijiji cha Lwandeti kimekuwa kama kielelezo cha makosa ya sarufi katika vipengele vya mofolojia na semantiki yahusuyo ujifunzwaji wa Kiswahili yatokanayo na Sheng’ katika muktadha wa vijijini nchini Kenya.

### 1.3 MASWALI YA UTAFITI.

Kutokana na malengo ya utafiti huu, utafiti huu umelenga kujibu maswali yafuatayo:-

(i) Je, Sheng' husababisha kwa kiasi gani matatizo ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na ya kisemantiki miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili walio Watachoni kutoka lokesheni ya Lwandeti?

(ii) Je, ni msambao upi uliopo wa makosa ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na kisemantiki baina ya wanafunzi wa vidato mbalimbali miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili walio Watachoni kutoka lokesheni ya Lwandeti kutokana na athari za Sheng'?

(iii) Je, vyanzo vya makosa ya kisarufi yafanywayo na wanafunzi wa Kitachoni katika vipengele vya mofolojia na semantiki kutokana na athari za Sheng' ni vipi?

### 1.4 MALENGO YA UTAFITI

(i) Kuchunguza ni kwa kiasi gani Sheng' husababisha matatizo ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na kisemantiki miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wanaozungumza Kitachoni kama lugha yao ya kwanza.

(ii) Kubaini msambao wa makosa ya kisarufi katika vipengele vya mofolojia na semantiki uliopo kutokana na Sheng' miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili Sheng' walio wa asili ya Kitachoni katika lokesheni ya Lwandeti.

(iii) Kudhihirisha vyanzo vya makosa ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na kisemantiki yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili walio Watachoni kutokana na athari za Sheng'.

### 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Kama walivyodai watafiti wa awali, Sheng' ni lugha msimu ya Kiswahili inayokua na kusambaa kwa kasi sana na hutumiwa haswa na vijana kama kitambulisho chao. Ni wazi kuwa jinsi lugha hii kipindi inavyokua na kusambaa kwa haraka athari zake zinaenea pakubwa. Na ni kutokana na hili ndipo tukapata msukumo wa kutathmini athari za lugha kipindi hii ya Sheng' katika utendaji wa wanafunzi Watachoni katika Kiswahili sanifu ambao ni wa shule za sekondari katika mazingira ya vijijini. Utafiti huu wa sasa umetambua kuwa Sheng' haitumiwi tu mijini bali na

vijijini pia. Kwa hali hii, utafiti huu wa sasa unakuwa muhimu kwani umeonyesha kiasi cha athari za Sheng' katika muktadha wa vijijini huku lokesheni ya Lwandeti ikirejelewa.

Utafiti huu wetu umekuwa wa manufaa kwa walimu wanaofunza somo hili la Kiswahili katika lokesheni hii ya Lwandeti kwa kuwa umewawezesha wao kujua na kutambua athari za Sheng' katika ufundishaji wa somo la Kiswahili katika kijiji hiki kwa kujikita katika vipengele vya mofolojia na semantiki. Ikumbukwe kuwa lokesheni ya Lwandeti inapatikana katika maeneo ya mashambani na vijijini, na kwa hivyo matokeo ya utafiti huu wa sasa umewafaa walimu na wanafunzi ambao mazingira yao ya ujifunzaji wa Kiswahili ni kama yale ya wale wa Lwandeti. Matokeo ya utafiti huu yameifaa hasa lokesheni ya Lwandeti kimsamiati japo suala hili li nje ya upeo na mipaka ya utafiti huu wa sasa. Hii ni kutokana na utafiti wetu wa awali ambao umeelekea katika kuonyesha kuwa kuna uwezekano wa leksemu za Sheng' ambazo hutumiwa na wanafunzi Watachoni katika shule zilizoko katika lokesheni ya Lwandeti kutumika katika maeneo ya Lwandeti na kwa Watachoni pekee. Kwa misingi ya hali hii, hali ya kuwepo kwa matokeo yasiyo mazuri katika somo hili la Kiswahili katika shule hizi kutokana na athari za Sheng' zilizo za kimofolojia na kisemantiki imeweza kubainishwa. Sababu kuu ya kuchagua lokesheni ya Lwandeti kwa utafiti wa athari za Sheng' kwa Kiswahili ni kuwa ni sehemu ambayo watu hujumuika kwa shughuli tofauti tofauti zikiwemo elimu. Kwa misingi hii pana uwezekano wa matokeo ya utafiti huu kudhihirika katika shule zingine za maeneo haya ya mashambani.

Tumechagua kushughulikia shule za upili kwa kuwa ni kiwango muhimu katika mfumo wa elimu wa 8-4-4 nchini Kenya ambapo Kiswahili hufunzwa na kutahiniwa kama somo la lazima. Isitoshe, kwa kuwa kuna hali ya mwendelezo na mwingiliano baina ya wanafunzi katika vidato tofauti katika sekondari, imekuwa vyema kuufanya utafiti huu ili kubaini msambao wa makosa ya Kiswahili kutokana na athari za Sheng'.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Katika utafiti wetu, tumejikita hasa katika kujifunza kwa Kiswahili ambacho ni sanifu na kinachofundishwa shuleni na walimu ambao wamehitimu kutoka vyuoni na vile vile kile kinachosomwa vitabuni – hasa vile vilivyoidhinishwa na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala ya Kenya na pia kuchapishwa na vyumba au mashirika ya uchapishaji vitabu tajika

Tumejikita hasa kwa wanafunzi wa Kiswahili katika shule za sekondari katika lokesheni ya Lwandeti ipatikanayo katika kaunti ya Kakamega lakini wazungumzao Kitachoni kama lugha yao asilia au ya kwanza.

Uteuzi wa wanafunzi wa shule za sekondari umefanywa kimaksudi kwa kuwa kihali halisi hawa ni vijana walio na uwezo wa kujifunza kirahisi lugha ya pili au hata ya tatu kinyume na watu wa makamo na wazee.

Lokesheni ya Lwandeti imechaguliwa vile vile kimaksudi ikizingatiwa kuwa kunao Watachoni wapatikanao Webuye ambayo ni mazingira ya mjini. Tafiti nyingi za hapo awali zimeiambatisha lugha ya Sheng' na mazingira ya mijini kukiwemo Kachipela (2014) na Mekonge (2016). Utafiti huu wetu umelenga ama kukubaliana au kutofautiana na matokeo ya tafiti za awali kuhusu athari za Sheng' kwa ujifunzaji mwema wa lugha ya Kiswahili.

Kwa sababu ya suala la upeo na mipaka, tumetumia shule tatu za upili kama shule vielelezo vya ujifunzaji wa Kiswahili kutokana na athari za Sheng' katika muktadha wa mashambani au vijijini. Utafiti huu wetu umekusudia kuchunguza na kutathmini iwapo lugha kipindi ya Sheng' husababisha makosa ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za wanafunzi wa Kiswahili ambazo zimeandikwa katika shule za upili katika lokesheni ya Lwandeti ambazo ni shule ya upili ya Maturu, shule ya upili ya Lukhokho na shule ya upili ya Lwandeti D.E.B. Hii ni kwa sababu katika tafiti zilizo za kimakadirio kama huu wa sasa ni vigumu kujumuisha kila mtu katika utafiti.Vilevile, kipengele cha kisarufi kilicho cha kisintaksia kimeachwa nje kimaksudi kwa sababu taaluma ya Isimu-historia-linganishi imebaini kuwa hiki ni kipengele cha kisarufi ambacho hakibadiliki kirahisi hasa katika lugha zilizo za mnasaba mmoja au zinazohusiana kwa karibu. Hapa, ni vyema kukumbuka kuwa Sheng' ikiwa ni lugha kipindi ya Kiswahili italandana na Kiswahili katika kipengele hiki cha kisarufi.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti huu umetumia nadharia ya Lugha Kadirifu ambayo iliasisiwa na Selinker (1969)

### 1.7.1. Nadharia ya Lugha Kadirifu

Selinker (1969) anasema kuwa Lugha Kadirifu ni lugha ambayo wanaojifunza lugha ngeni huunda kutokana na ujuzi walionao katika lugha yao ya kwanza .Lugha hii kadirifu huwa kati ya

lugha ya wazungumzaji ya kwanza na lugha lengwa. Mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili hufanya makosa mbalimbali katika ujifunzaji wake mpaka anapofikia kiwango cha kuimarika katika lugha hiyo. Selinker alibainisha sifa za lugha kadirifu kuwa: watu wanapoitumia lugha sheria za lugha hiyo hubadilika badilika, lugha hii kadirifu huwa na uwezo wa kukua kadiri mtu anaitumia lugha hiyo, na pia lugha kadirifu hutumika kutegemea mazingira aliyomo mzungumzaji

Selinker (ibid) anaelezea kuwa kuna mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo mzungumzaji anaweza kutumia katika kuchanganua makosa anapoitumia lugha. Mifanyiko hii ni kama ifutavyo:

I. Kuhamisha kwa sheria za lugha ya kwanza ambapo mzungumzaji hutumia sheria, vifaa na mifumo ya lugha ya kwanza katika lugha lengwa.
II. Kujumlisha kanuni au sheria za lugha lengwa ambapo mtumizi wa lugha lengwa hutumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili.
III. Uhamisho katika ufundishaji na mikakati wa mawasiliano katika lugha ya mzawa wa lugha ya pili au mtumizi wa lugha anayeifahamu lugha hiyo barabara na pia anayejifunza lugha hiyo.
IV. Mbinu anazotumia katika kujifunza za kurahisisha mfumo wa lugha ya pili kwa kupunguza uziada wa hiyo lugha hasa kwa upande wa semantiki.
V. Athari ambazo hutokana na mbinu zinazotumika katika kufunza. Hili hutokea wakati mtumizi wa lugha ya pili huitumia kutokana na kujifundisha ambako sio sahihi.

Nadharia ya Lugha Kadirifu inahusu umilisi wa lugha na tofauti zake kutegemea kanuni za lugha na sheria za lugha ya kwanza mintarafu lugha lengwa. Hivyo nadharia hii imetusaidia kutambua vyanzo vya makosa katika lugha na maandishi ambayo wanafunzi wa sekondari hutumia haswa katika insha zao na athari za lugha nyingine ambapo katika muktadha wa utafiti huu ni athari za Sheng' kwa Kiswahili.

## 1.8. YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Sheng’ ni lugha kipindi ambayo hubadilika mara kwa mara. Kwa mujibu wa Mukhwana (2014), Sheng’ ina msamiati mpana. Uzito wa hoja hii inatiliwa mkazo kwa kutolea mifano mahsusi ya maneno yanayotumika katika Sheng’ kama vile “dem”,”manzi” na “chiki” kurejelea neno msichana. Mtaalam huyu anazidi kufafanua kuwa Sheng’ hutumia usafidi mwingi ambapo usafidi huu huwa na maana ya kutumia lugha iliyo na wingi wa staha au kuficha ukali wa meneno. Mtazamo huu wa Mukhwana (2014) una ukweli kwa kuzingatia baadhi ya msamiati kama vile “kuro” kurejelea msichana kahaba au “juala” kurejelea “kondomu”. Ni bayana kuwa matumizi ya Sheng’ hupunguza makali wakati mzungumzaji anapozungumza kwa kurejelea mifano hii mahsusi. Lugha hii huweza kuhifadhi siri miongoni mwa watumizi wake. Kwa mujibu wa Mukhwana (2014) ametunufaisha kwa kina katika mchakato wa utafiti wetu katika kufasiri visawe vya lugha katika lugha msimu ya Sheng’.

Baadhi ya wasomi wengine walioshughulikia mada hii ya Sheng’ ni Buliba na wenzake (2006).Wanashikilia kwamba lugha hii kipindi ya Sheng’ ni zao la mwingiliano baina ya makabila mbalimbali nchini Kenya hususan wanaoishi mjini Nairobi na viungani mwake kama vile Jericho , Bahati na Kaloleni. Kulingana na wao, lugha ya Kiswahili na ile ya Sheng’ huwa na mshabaha. Ni kutokana na haya ambapo baadhi ya vijana wanahitajika kutumia mifumo ya Kiswahili sanifu katika kazi zao aghalabu katika maandishi huchanganyikiwa na jambo hili ambalo lina mchango anuwai kwetu kama watafiti kutambua usuli wa lugha ya Sheng’. Licha ya hayo lengo kuu la mchakato wa utafiti wa sasa si chanzo cha Sheng’ kama lugha ila athari zake miongoni mwa watumizi wa Kiswahili kama vile Watachoni wa lokesheni ya Lwandeti. Maoni ya wataalam hawa yametusaidia katika mchakato wa utafiti wa sasa katika kubaini iwapo muundo wa Sheng’ unaosemekana kwamba unaegemezwa kwa Kiswahili ambacho ni Kibantu unaafikiana na ule wa Kitachoni au la. Hii imetuwezesha kuliweka dhahiri swala la asili ya Kitachoni ambalo limezua mjadala ila lipo nje ya mchakato huu wa utafiti.

Kutokana na tofauti za kileksia, Sheng’ hubainisha vikundi ambavyo ni vidogo vidogo vya watu wanaotumia Sheng’ kwa mujibu wa Githinji (2006). Kutokana na mashiko kutoka hoja hii kazi yake imekuwa mwafaka katika utafiti wetu kwa vile imechangia pakubwa katika kubainisha miundo tofauti tofauti ya Sheng’. Mawazo haya ya Githinji (2006) yameufanya utafiti wetu kuwa halali kwa vile yameashiria kuwa Kitachoni cha mjini kinaweza kuwa na tofauti nyingi na kile

cha vijijini kwa sababu Vitachoni vyote viwili vimeathiriwa na Sheng' katika mchakato mzima wa ufasiri na ujifunzaji wa Kiswahili.

Kwa mujibu wa Mazrui (1995) anazidi kutilia msisitizo kwamba Sheng' ni lugha msimu itumiwayo na vijana wanaotoka katika jamii zilizokumbwa na uchochole au watu kutoka tabaka la kimaskini na wale ambao wametoka Nairobi na hivyo basi kutumika kama mbinu ya kuwatenga hawa wa kimaskini na wale wa kitajiri. Mawazo sawia yamedokezwa na Osinde (1987). Kazi hii ya Mazrui ni faafu kwa vile imetupa uwezo wa kufahamu mapisi ya Sheng' kwa kuangazia kuzuka kwake. Nia ya utafiti wa sasa si kubaini chanzo cha Sheng'. Kutokana na tafiti tangulizi zilizoonyesha maenezi ya Sheng' nchini Kenya, mchakato wa utafiti wa sasa unadhamiria kuonyesha athari za Sheng' katika ujifunzaji wa Kiswahili katika mazingira ya vijijini. Kwa kiwango kimoja mawazo ya Mazrui yamekinzana kutokana na kipindi kirefu kilichopita na utafiti huu wa sasa.

Lugha kipindi ya Sheng' inahusishwa na makundi ya watu ambao hufanya maovu kinyume na maadili ya jamii wanamoishi kwa mujibu wa Mukwana (2014) na Mahu (2009). Ulanguzi wa afyuni, ubakaji na uporaji ni baadhi ya matendo ambayo ni kinyume kulingana na maadili. Madai haya yanapotosha Kwa vile Sheng' huwa na tauria nyingi kama zilivyobainishwa awali. Kazi hizi zimechangia mno katika kubaini mielekeo na mitazamo ya walimu wanaofundisha katika shule na upili ambazo tumeteua katika kufanyia utafiti huu kuhusu Sheng' na ni kutokana na athari hizi ambazo zimekuwa chanya au hasi katika kujifunza na kufunza lugha ya Kiswahili katika lokesheni ya Lwandeti ambapo imebainishwa na wanafunzi pamoja na walimu ambao ni washika dau katika suala la ufundishaji wa Kiswahili sanifu. Tafiti hizi za Mahu na Mukhwana zimechukulia Sheng' kuwa hifadhi ya vijana wa mjini. Kutokana na utafiti wa awali hii ni kinyume na uhalisia uliofanywa na mtafiti katika lokesheni ya lwandeti. Utafiti wa awali ulionyesha kwamba lugha ya Sheng' imeenea kote nchini Kenya. Katika kijiji kama vile Lwandeti usimbeko na utovu wa maadili ni maswala yanayokashifiwa na jamii ambayo hayawezi kuruhusiwa kamwe. Kwa hivyo kazi ya Mahu na Mukwana zimekuwa tofauti na kazi ya sasa.

Mekonge (2016) ni mtaalam mwingine ambaye ameshughulikia suala la Sheng' katika elimu. Utafiti wake ulihusu athari ya Sheng' katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili za Gusii. Tafiti za Mekonge zimekuwa na mchango mkubwa sana kwa utafiti wetu ambao

umeelekea kutafiti athari za Sheng’ zilizo za kisemantiki na za kimofolojia na uchunguzi wake umeegemea vile vile katika semantiki na mofolojia. Hata hivyo, kazi ya mtaalam huyu iliegemea katika mandhari ya mjini kinyume na kazi ya sasa ambayo imekita mihimili yake vijijini. Utafiti huu wa sasa umefaidi kutoka na kazi ya Mekonge katika suala la mahusiko ya natharia aliyoifasiri awali ya lugha kadirifu ya Selinker (1969).

### 1.8.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Athari za Sheng’ kwa Lugha ya Kiswahili.

Okoto (2015) anasema kuwa lugha ya Sheng’ hutumia maneno ambayo yamkinika ni sahihi katika Kiswahili sanifu na kwa hiyo kutokana na mitazamo hasi ya watu ambao hawaitumii lugha ya Sheng’ huwafanya watu wengine kuacha kuyatumia maneno haya. Tukitolea mfano wa maneno yaliyotumika katika lugha ya Sheng’ na ambayo ni Kiswahili sanifu ni kama neno ‘demu’ ambalo ni neno linalomaanisha aina ya nguo na hususan kitambaa cha watu wa jinsia ya kike kinachotumiwa kufungia maziwa yao haswa wanapolima na kwa upande mwingine neno hili katika Sheng’ lina maana ya mtu mwenye jinsia ya kike. Pia, Sheng’ hutumia neno lingine kama ‘Kuro’ na ambalo katika Kiswahili sanifu lina maana ya mnyama anayeishi porini na ambaye kwa kiwango kikubwa anafanana na Kulungu ila katika kijilugha cha Sheng’ humaanisha mtu kahaba. Vile vile mfano mwingine wa neno la Sheng’ na ambalo ni Kiswahili sanifu ni neno ‘mbuyu’ ambalo hutumika katika Sheng’ kwa maana ya baba mzazi badala ya maana asilia ya “Mti fulani mkubwa wenye kuzaa mabuyu”. Hali hii imeashiria kuwa Sheng’ kama lugha kipindi ya Kiswahili inao uwezo wa kupotosha maana halisi ya maneno ya Kiswahili. Maoni haya ya Okoto kuhusu Sheng’ yamekuwa kama msingi wa kazi yetu ya utafiti kwa kuwa yametuongoza kwa namna ambavyo neno la kawaida katika Kiswahili huweza kupewa maana ya ziada au tofauti katika lugha ya Sheng’ kusudi likiwa ni kuipambanua Sheng’ kama lugha inayojisimamssia. Hali hii imetusaidia kuangazia athari za Sheng’ katika ujifunzaji ufaao wa Kiswahili miongoni mwa Watachoni waishio katika lokesheni ya Lwandeti na walio katika shule za sekondari.

Naye Odhiambo (2013) aliangazia katika utafiti wake utofauti ambao hutokea miongoni mwa watu ambao ni waaminifu katika maabadi na ambao ni wazee na wale ambao ni vijana. Alieleza kuwa wengi wa wazee hawaelewi matumizi ya lugha ya Sheng’ ikilinganishwa na vijana ambao wanaielewa vizuri. Mwandishi huyu alipendekeza kuwa waumini hawa hutumia nyimbo katika

ibada yao ambazo zimesheheni misamiati ya lugha ya Sheng’. Utafiti huu wa Odhiambo (2013) umekuwa na manufaa makubwa katika kazi yetu kwani mwandishi huyu aliangazia athari za lugha kipindi ya Sheng’ kwa dini ya wakristo ilhali utafiti huu wetu unaangazia athari za Sheng’ katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za lokesheni ya Lwandeti katika kaunti ya Kakamega. Kwa misingi hii, kazi hizi mbili zimetofautiana katika misingi ya mandhari, malengo na upeo.

Kachipela (2014) naye amechunguza makosa mbalimbali wanayofanya wanafunzi katika shule za msingi katika kazi zao za Kiswahili na ambayo husababisha matokeo yasiyoridhisha katika mtihani wa somo la Kiswahili. Utafiti wake uliokitwa katika kaunti ndogo ya Westlands jijini Nairobi unaonyesha kuwa Sheng’ huathiri utendaji wa wanafunzi katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa. Utafiti wake ni wa upeo tofauti na wetu kwani wetu ni wa kiwango cha shule za upili katika lokesheni ya Lwandeti katika kaunti ya Kakamega. Mapendekezo yake yametufaa kwani alipendekeza tafiti kuhusu athari za Sheng’ katika shule za upili na vyuo zifanywe. Hivyo utafiti wake umekuwa msingi bora wa tatizo letu la utafiti. Isitoshe, kazi ya Kachipela ilijikita hasa katika mtaa wa mabanda wa Kangemi jijini Nairobi kinyume na kazi hii ya sasa ambayo imejikita katika muktadha wa vijijini katika lokesheni ya Lwandeti na kwa kulenga jamii lugha moja ya Kitachoni.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

Matamshi ya wahusika pamoja na insha ambazo zimekuwa zimeandikwa na wanafunzi wa Kiswahili kutoka katika shule ambazo tumeteua za sekondari miongoni mwa wazungumzaji wa Kitachoni ndizo tumetumia kama data yetu ya kimsingi katika utafiti huu wetu. Kisha baada ya kukusanya data hiyo tumefuata utaratibu maalum ili kuyafikia malengo yetu ya utafiti na kwa kuwa utafiti huu wetu umekuwa ni wa kiufafanuzi, tumeichanganua data ambayo tumekuwa tumeikusanya jinsi ilivyo. Utaratibu ambao tumeufuata katika kuangalia suala zima la mbinu za utafiti umekuwa ufuatao;

1. Mbinu ambazo tumetumia katika kukusanya data

2. Vifaa ambavyo tunahitaji katika utafiti wetu.

3. Mbinu ambazo tumetumia kuichanganua na kuiwasilisha data yetu na,

4. Namna tumeyahifadhi maadili yetu katika utafiti

### 1.9.1 Mbinu za Kukusanya Data

Insha ambazo ambazo tumewapa wanafunzi wateule wa Kitachoni kutoka katika Lokesheni ya Lwandeti kuandika ndizo zimekuwa data yetu ya kimsingi katika utafiti wetu. Pili, tumekuwa tukitalii maandishi mbalimbali kutoka katika maktaba ili tuweze kubaini yale ambayo yameandikwa kuhusu mada yetu na pia tuweze kutambua ni nadharia ipi ilikuwa mwafaka kwa utafiti wetu huku tukitilia maanani maswali ya utafiti wetu pamoja na malengo yetu ya utafiti. Tumetazamia kutekeleza uchunguzi huu wetu kifani ambapo shule katika lokesheni ya Lwandeti ndizo tumetumia kupata data. Shule hizi ni pamoja na shule ya upili ya Maturu, shule ya upili ya Lukhokho na shule ya upili ya Lwandeti D.E.B. Uchaguzi wa shule hizi umechochewa na kuwepo kwa matokeo yasiyoridhisha katika Kiswahili katika mitihani ya kitaifa katika miaka ya hivi karibuni. Tumewahoji walimu ana kwa ana ili kupata maoni na mielekeo ya walimu kuhusu athari za Sheng' katika ufundishaji wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu athari za Sheng' kwa ufundishaji wa Kiswahili huweza kuwagusa walimu kwa njia ya moja kwa moja, wao wakiwa ni wadau wakuu mojawapo. Insha ambazo tumewapa wanafunzi zimekuwa za kiubunifu na ni sehemu muhimu kwenye silabasi za shule za upili nchini Kenya inayohitaji kufunzwa na pia kutahiniwa.

Tumekuwa tukiteua jumla ya wanafunzi kumi kutoka kila shule na wakiwa ni wa jinsia zote mbili yaani kike na kiume. Idadi ya watafitiwa imeafikiwa kimaksudi huku mtafiti akiamini kuwa idadi hii itatoa data inayostahili.

Mtafiti pia ni mzungumzaji asilia wa Kitachoni, mwanafunzi wa Kiswahili,na anayeifahamu lugha ya Sheng'. Kutokana na hali hii, mbinu nyingine ya ukusanyaji data kwa ajili ya utafiti huu imehusu uchunguzi shiriki.

### 1.9.2 . Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti ambavyo tumevitumia ni pamoja na kijitabu kidogo cha kuandikia, kalamu ya kunukuu, pamoja na kinasasuti.

### 1.9.3. Mbinu za Kuchanganua na Kuwasilisha Data.

Sisi kama watafiti tumehakikisha kuwa tumewapa wanafunzi insha ambazo ni za kiubunifu ili waweze kuandika kisha baada ya kuzikusanya insha hizo na kuzisahihisha tumekuwa tukiyatambua makosa ambayo wanafunzi hawa wamekuwa wameyaandika halafu tumehakikisha kuwa tumeyagawa makosa ambayo yamefanywa katika kategoria za makosa ya kimofolojia na makosa ya kisemantiki kulingana na kidato ambamo mwanafunzi huyu anasoma, na tumekuwa tukitumia nadharia iliyopendekezwa na Selinker (1969) ya uchanganuzi makosa katika kuichanganua data ambayo tumekuwa tumeikusanya. Baada ya kufanya hivyo, tumebainisha ni nini chanzo cha makosa hayo ya mwanafunzi na kuyarekebisha kwa kumuonyesha mwanafunzi huyo majibu katika karatasi yake. Makosa ambayo sisi kama watafiti tumekuwa tumeyapigia mstari ndiyo yaliyodhihirisha athari za lugha kipindi ya Sheng’ katika ufundishaji wa Kiswahili miongoni mwa watu wazungumzao Kitachoni katika Lokesheni ya Lwandeti.

Baada ya kutambua makosa haya tumeweza kuripoti kinathari na kwa mijadala baina yetu na wanafunzi na walimu huku tukizingatia nadharia ambayo tumetumia pia huku tukitilia maanani maswali yetu ya utafiti kuhusu “Athari za Sheng’ kwa Ufundishaji wa Kiswahili miongoni mwa Watachoni katika lokesheni ya Lwandeti”.

### 1.9.4 Maadili katika utafiti

Kabla ya kwenda nyanjani kwa ajili ya ukusanyaji data tulipata barua za kututambulisha kama wanafunzi na watafiti kutoka kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Nairobi na kitengo kinachohusika na utoaji vibali katika serikali kuu jijini Nairobi. Nyanjani tumewahakikishia watafitiwa kuwa data ambayo tumekusanya imetumika kwa shughuli za kiakademia pekee na wala si kwa shughuli nyingine yoyote ile. Pia, tumehakikishia watafitiwa usiri wao kwa kutotumia majina yao bali nambari katika insha ambazo wametuandikia kwa ajili ya utafiti huu.

## 1.10 HITIMISHO.

Katika sura hii, tumeangazia masuala mbalimbali yakiwemo usuli wa mada ambapo tumeangazia ni kwa namna gani lugha ya Sheng' ambayo ilichukuliwa kuwa ya mjini kwa sasa imeenea na kutumiwa vijijini pia. Tatizo la utafiti letu limekuwa ni kwa namna gani lugha hii ya Sheng' imechangia katika kudorora kwa viwango vya kupasi mitihani haswa ule wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa lokesheni ya Lwandeti haswa katika kuzingatia kipengele cha kimofolojia na kisemantiki. Tumeonyesha pia maswali na malengo ya utafiti wetu, na pia kuonyesha sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa kinadharia ambapo tumeegemea nadharia ya lugha kadirifu ya Selinker (1969), pia tumeeleza kuhusu yale yaliyoandikwa kuhusu mada na yale yaliyoandikwa kuhusu lugha ya Sheng'. Vifaa vya kukusanya data na namna ya kuchanganua data yetu pia vilionyeshwa. Mwisho, utafiti huu umezingatia maadili ambapo tumewahakikishia watafitiwa wetu kuwa data ambayo tumekuwa tukikusanya imetumika kwa shughuli za kiakademia pekee hivyo tukawahakikishia usiri wao kwa kutumia nambari badala ya majina yao tukiwa nyanjani.

## SURA YA PILI

## 2.0. MBINU ZINAZOTUMIKA KATIKA KUUNDA LEKSEMU ZA LUGHA YA SHENG'

### 2.1. Utangulizi

Sura hii imeangazia uundaji wa leksimu katika lugha ya Sheng' kwa kuangazia muundo wa kimofolojia na kisemantiki unaoendana na msamiati wa lugha ya Sheng' na ambao ndio husababisha makosa katika lugha sanifu ya Kiswahili. Athari za makosa haya zimejitokeza katika baadhi ya insha ambazo zimeandikwa na wanafunzi walio katika shule za upili tukirejelea lokesheni ya Lwandeti. Utafiti huu unakubaliana na ule wa Ogechi (2002) anapodai kuwa lugha hii ya Sheng' hupata msamiati wake kutoka lugha tofauti tofauti na hivyo mabadiliko mbalimbali huwa yanatokea wakati wa kutumia misamiati hii. Utafiti huu wetu umeonyesha kuwa mofolojia hutumika katika kuunda leksimu za Sheng' jinsi inavyotumika katika uundaj wa leksemu za lugha nyingine yoyote ile. Kwa ufupi mbinu zinazotumika katika kuziunda leksemu za Sheng' ni pamoja na akronimu, ubadilishaji silabi, upolisemia, ubunaji, ukatizaji, unyumbuzi kapa, ukopaji, onomatopia, uhulutishaji na ujenzi ghairi. Hapa chini tumefafanua mbinu hizi na kuweza kuonyesha jinsi zimeathiri insha za watafitiwa wetu.

### 2.2 MBINU ZA KUUNDA LEKSEMU ZA SHENG'

#### 2.2.1 Uambishaji

Kama anavyoeleza Mweri (2010), uambishaji hali ya kuvipachika viambishi katika mzizi wa neno wakati wa kuunda maneno mapya.

Katika Kiswahili tumepata mifano ifuatayo:

| **Uambishaji** | **Leksemu undwa** |
|---|---|
| M+jenzi | Mjenzi |
| M+ti | Mti |
| Kiji+tabu | Kijitabu |

| | |
|---|---|
| Ku+cheka | Kucheka |

Tukirejelea mifano ya maneno tuliyotumia hapo juu, mbinu ya unominishaji imedhihirika katika viambishi tulivyotumia katika maneno 'mjenzi', 'mti', na 'kucheka.' ilhali neo kitabu limedunishwa au kuonyesha udogo kwa kutumia kiambishi kiji- .

Lugha msimu ya Sheng' pia imetumia mbinu hii ya uambishaji katika kujiundia leksimu na ifuatayo ni baadhi ya mifano ambayo ilijitokeza katika kazi za watafitiwa wetu.

| **Uambishaji** | **Leksimu undwa** | **Maana** |
|---|---|---|
| Ka+demu | Kademu | Mtu wa jinsia ya kike |
| Ma+jamaa | Majamaa | Wanaume wengi |
| Vi+nice | Vinice | Vyema |
| Ma+mode | Mamode | Walimu wengi |
| Ka+nairoo | Kanairoo | Mji wa Nairobi |

Maana mbalimbali imejitokeza kutokana na matumizi ya viambishi vilivyotumika katika mifano ya maneno tuliyotumia hapo juu na ambayo ni {ka} katika 'kademu' kwa kuashiria udogo au udunishaji na {vi-} katika 'vinice' kuashiria kielezi cha kufanya jambo vyema na neno 'nice' ni la asili ya Kiingereza na limepata maana ambayo ni mpya baada ya kufanyiwa upanuzi katika lugha ya Sheng'.

### 2.2.2 Ukatizaji

Kama wanavyoeleza Iribemwangi na Mukhwana 2011, Ukatizaji ni mbinu ya kufupisha ili kuunda vifungu au maneno mapya. Naye Ogechi (2005), anaelezea kuwa ukatizaji ni ufupishaji wa kudondosha silabi aidha moja au zaidi katika kuunda maneno.Ukatizaji hujikita haswa katika kuhawilisha neno ambalo ni la kukopa halafu hulikata neno hilo na kuliongezea viambishi ama mwanzoni (viambishi awali) au mwishoni (viambishi tamati) katika mzizi wa neno ili kuunda leksimu za Sheng'. Ukatizaji awali umejitokeza katika mifano ifuatayo katika lugha sanifu ya Kiswahili.

| **Leksemu katwa** | **Leksemu asili** |
|---|---|
| Dkt. | Daktari |
| Mhe. | Mheshimiwa |
| Prof. | Profesa |

Kuna baadhi ya maneno katika Sheng' ambayo ymaeundwa kwa mbinu hii ijapokuwa maneno haya huwa yamekopwa na kutoholewa kisha kufanyiwa ukatizaji.

Mfano:

| **Leksemu katwa** | **Leksemu asili** |
|---|---|
| Kk. | Kakamega |
| Kti. | Kitui |
| Afu. | halafu |
| Btr. | Butere |

Mifano hii ya maneno inadhihirisha ukatizaji ambao ni wa mwanzoni mwa neno au mwishoni mwa maneno. Mifano hii ilijitokeza katika insha za watafitiwa wetu na kwa hiyo ilikuwa ni athari ya lugha ya Sheng'kwa Kiswahili katika insha ambazo tumezisahihisha. Makosa ya aina hii yamekuwa asilimia ya chini.

### 2.2.3 Unyambulishaji

Unyambulishaji ni mbinu ya kuunda maneno mapya ambapo viambishi hupachikwa mwishoni mwa shina la neno na kuzua maana tofauti na maana asili hivyo kuunda misamiati mipya.

Kwa mfano;

| **Unyambulishaji** | **Leksemu undwa** |
|---|---|
| Andik-iw-a | Andikiwa |
| Lamb-an-a | Lambana |
| Pat-an-ish-a | Patanisha |

| | |
|---|---|
| Chez-esh-a | Chezesha |
| Ruk-w-a | Rukwa |

Tukirejelea mifano ya maneno tuliyoitoa hapo juu, viambishi tamati vimetumika katika kudokeza minyambuliko mbali mbali ya leksimu hizi. Katika maneno ‘andikiwa’ na ‘rukwa’, -iw-, na –w- inaashiria mnyambuliko wa kutendewa au kufanyiwa ilhali kauli ya kutendana inajitokeza katika maneno ‘lambana’ na ‘patanishwa’ ambapo kiambishi -an- kimetumika. Na kwa upande mwingine viambishi –ish- na –esh- vimetumika kuonyesha kauli ya kutendesha katika maneno ‘patanisha’ na ‘chezesha’.

Lugha ya Sheng’ imetumia mbinu ya utohozi katika kujiundia leksemu zake kama ilivyojitokeza katika insha za watafitiwa kama matatizo ya kisarufi yaliyo ya kimolojia na kisemantiki.

Kwa mfano;

| **Unyambuaji** | **Leksimu undwa** | **Maana** |
|---|---|---|
| Piti-li-zi-a | Pitilizia | Kuzidi kiwango |
| Pita-nga | Pitanga | Pita mara kwa mara |
| Onge-le-a | Ongelea | Sema mara kwa mara |
| Huwa-nga | Huwanga | Mara kwa mara |
| Ishi-a | Ishia | Ondoka |
| Utawez-an-a | Utawezana | Utafaulu |

Katika mifano tuliyotoa hapo juu, neno ‘pitanga’ kiambishi {nga} kimetumika kuwakilisha hali ya kufanya kitendo hiki mara kwa mara, huku kiambishi {le} katika ‘ongelea’ kinazua dhana ya kufanyiwa ama kutendewa jambo fulani. Insha za watafitiwa pia zilijitokeza na maumbo ya aina hii ambapo kwetu hii ni athari ya Sheng’ kwa Kiswahili sanifu.

### 2.2.4 Onomatopia

Kama wanavyodai Iribemwangi na Mukhwana (2011) Onomatopia ni kuwa ni miigo au yaweza kuwa pia ni milio ya sauti inayotumika katika kuundia maneno haswa kwa kutumia kigezo cha uamilifu, sauti umbo na milio ya vitu mbalimbali katika ulimwengu.

Mfano katika lugha rasmi ya Kiswahili,

| **Leksemu undwa** | **Maana** |
|---|---|
| Tuktuk | Kifaa kinachotumiwa kwa usafiri kinachofanana na pikipiki ila kina magurudumu tatu. |
| Tingatinga | Trekta ambayo ni kubwa |
| Pikipiki/Kitutu | Chombo cha magurudumu mawili cha usafiri ambacho katika kwenda hujitokeza na sauti tututu |
| Kipaza sauti | Kifaa cha kupaza sauti na kufanya usikike vyema. |

Kwa kuzingatia kigezo cha uamilifu, neno kipaza sauti ni mwafaka kwa kuwa utendakazi wake unaliafiki kwani chombo hiki hutumika katika kupaza sauti. Kwa upande mwingine, maneno kama vile Tuk tuk, Tingatinga na Pikipiki yameundwa kutokana na milio ambayo vifaa hivi hutoa wakati vinapoendeshwa.

Lugha ya Sheng' vile vile ina uwezo wa kujiundia maneno yake kwa kuitumia mbinu hii ya Onomatopia. Insha za watafitiwa wetu zimejitokeza na msamiati wa aina hii na hali hii ilidokeza athari au chanzo cha makosa kwa Kiswahili sanifu. Hii ni kumaanisha kuwa lugha ya Sheng' huweza kujiundia msamiati wa kionamatopea ambao unachukuliwa na wasemaji wake wakidhani kuwa Kiswahili sanifu.

Kwa mfano,

| **Leksemu undwa** | **Maana** |
|---|---|
| Kaacha | Kutiwa pingu |
| Kidi | Bunduki |
| Brrcha | Kuleta matatizo |

### 2.2.5 Upolisemia

Obuchi na Mukhwana (2010) wanaeleza kuwa Upolisemia ni ile hali ya kuongezea kwa maneno maana zaidi. Maneno haya yanaweza kupewa upanuzi kwa kutajia dhana ngeni ambayo haina jinsi ya kuitaja katika lugha pokezi. Kiswahili vilevile kimetumia mbinu hii.

Kwa mfano,

| Neno | Maana asili | Maana ya ziada |
|---|---|---|
| Taa | Kifaa kinachotoa mwangaza | Samaki mkubwa |
| Tai | Aina ya ndege ambaye ni mkubwa | kitambaa cha kufungwa shingoni |
| Koo | Sehemu fulani ya mwili | Kuku wa kike |
| Mbuzi | Mnyama wa kufugwa nyumbani | Kifaa kitumiwacho kukunia nazi |

Matatizo ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na kisemantiki yalibainika katika insha za Kiswahili zilizoandikwa na watafitiwa wetu. Hili lilitokana na athari za Sheng' kwa Kiswahili sanifu.

Kwa mfano,

| Neno | Maana asili | Maana ziada |
|---|---|---|
| Form | Karatasi ya maswali | Mpango fulani |
| Donda | Kondakta wa gari | Kidonda |

### 2.2.6 Ubunaji

Hii ni mbinu inayotumika katika uundaji wa maneno mapya na ambayo hutokana na hali ya uchochezi na uvumbuzi ambao ni mpya wa kisayansi. Kwa kurejelea lugha ya Kiswahili tumepata msamiati ufuatao;

| Leksemu undwa | Maana |
|---|---|
| Barakoa | Kitambaa cha kuziba pua na kinywa ili kuzuia virusi |
| Kitukusi | Kifaa ambacho hutumiwa kukata kucha |
| Uyoka | Kifaa kitumiwacho kupima wagonjwa wa Saratani |

Leksimu pia zinaweza kuundwa katika lugha kipindi ya Sheng' kwa kutumia mbinu hii ya ubunaji.

Mfano,

| **Leksimu undwa** | **Maana** |
|---|---|
| Ndeng'a | Bunduki |
| Ndai | Gari |
| Mdhiba | Rafiki wa kiume |

Maneno ya Sheng' tuliyotumia hayajakopwa kutoka lugha yoyote ila tu imetumika kutolea maana kwa msamiati wa Sheng'kulingana na miundo yake. Kutokana na data kutoka kwa watafitiwa, mbinu hii haikujitokeza sana na kwa hiyo kiwango chake cha athari za kimofolojia na kisemantiki kwa Kiswahili ni cha chini.

### 2.2.7 Akronimu

Akronimu huhusisha kuleta pamoja sehemu za mwanzo za maneno au vishazi ili kuunda maneno mapya (Obuchi na Mukhwana 2015). Kwa kawaida huwa inafupisha maelezo yaliyo marefu. Kwa kawaida maelezo ambayo ni marefu huwa yanafupishwa. Kwa kurejelea lugha ya Kiswahili tunapata mifano ifuatayo;

| **Maneno** | **Akronimu** |
|---|---|
| Ukosefu wa KInga MWIlini | UKIMWI |
| CHAkula cha JIOni | CHAJIO |
| CHAkula cha MCHAana | CHAMCHA |
| Wavu Wa Walimwengu | WWW |
| TAasisi ya TAaluma za KIswahili | TATAKI |
| HOMOni ya kiKE | HOMOKE |

Data yetu tuliyoikusanya iliyotokana na watafitiwa haikuonyesha neno lolote la Sheng' ambalo limeundwa kwa kutumia mbinu hii. Kwa hali hii tunaweza kusema kuwa mbinu hii haiathiri lugha ya Kiswahili sanifu.

### 2.2.8 Uhulutishaji.

Kwa mujibu wa wataalamu (Obuchi na Mukhwana 2010), mbinu hii ya uhulutishaji ni mbinu ya kuunganisha vipengele viwili ambavyo kihali halisi huwa havifai kuwa pamoja katika kuunda maneno mapya.

Mfano katika Kiswahili,

| **Neno awali** | **Neno undwa** |
|---|---|
| Chakula+cha+jioni | chajio |
| Chakula+cha +mchana | chamcha |
| Mfupa+wa+paja | fupaja |

Mbinu ya uhulutishaji haikujidhirisha katika data tuliyoipata kutokana na watafitiwa wetu.Kwa hali hii tunaweza kusema kuwa msambao wa uhulutishaji haupo katika lugha ya Sheng'

### 2.2.9 Uambatishaji

Uambatishaji ni hali ya kuyaunganisha maneno mawili au zaidi pamoja na maneno haya huwa huru kwa minajili ya kuunda maneno mapya ambayo yanasimamia wazo moja na ambayo hutamkwa kama neno moja. Maneno mapya ambayo huwa yameundwa huwa yanatofautiana kimaana na maneno asili.

Mfano:

| **Maana ya awali** | **Neno mwambatano** |
|---|---|
| Mama+sukari | Mamasukari |
| Bata+mzinga | Batamzinga |
| Mja+mzito | Mjamzito |
| Bata+mshenzi | Batamshenzi |

| | |
|---|---|
| Askari+kanzu | Askarikanzu |

Katika lugha ya Sheng' pia tulipata data ya aina hii katika kazi za watafitiwa wetu.

Mfano:

| **Maneno ya awali** | **Neno mwambatano** | **Maana** |
|---|---|---|
| Peng'+ting | Peng'ting' | Msichana mrembo |
| Dum+nacha | Dumnacha | Mchana yote |
| Bu+fee | Bufee | Nauli ya gari |

Maana ambayo ni ya asili ya neno huwa inapotea ilhali maneno unde na ambayo ni ya mwambatano hudokeza maana ambayo ni ya kileksia.

Kwa kutolea mifano hapo juu neno 'Bufee', 'Buu' ni neno la Sheng' linalomaanisha 'gari' ilhali neno 'fee' ni neno ambalo ni la Kiingereza kwa maana ya 'malipo.'

### 2.2.10 Ubadilishaji Silabi.

Ubadilishaji silabi ni mbinu ya kuunda maneno mapya kwa kupanga na kupangua silabi.

Maneno mapya huundwa kwa kufuata muundo wa kutokea sehemu ya nyuma hadi sehemu ya mbele kinyume na miundo ya kawaida iliyozoeleka (Ogechi 2005)

Mfano katika lugha ya Kiswahili sanifu ni kama ufuatao;

| **Leksimu undwa** | **Leksimu asili** |
|---|---|
| Nyie | enyi |

Mifano tuliyopata kutokana na data ya utafiti wetu ni kama ifuatayo;

| **Leksimu asili** | **Leksimu undwa** | **Leksimu changizi** |
|---|---|---|
| Desk | Skide | Kiingereza |
| Flat | Tfla | Kiingereza |
| Safi | Fisa | Kiswahili |

### 2.2.11 Ukopaji

Kama anavyodai mtaalamu Mweri (2010), ukopaji ni hali ya kuhamisha vipashio vya lugha kutoka katika lugha moja hadi nyingine. Lugha ambayo huwa imekopwa kwa kawaida huwa inajulikana kama lugha changizi ilhali kwa upande mwingine lugha ambayo huwa imekopa hujulikana kama lugha pokezi.

Aina za ukopaji ni kama vile:

#### 2.2.11.1 Ukopaji Utohozi

Ukopaji huu hudhihirika wakati ambapo neno hukopwa kutoka katika lugha changizi na kuhawilishwa ili lichukue umbo la lugha pokezi (Iribemwangi na Mukhwana 2011)

Uhawilishaji wa aina hii huweza kufasiriwa kama hali ambapo leksimu zinaweza kupata mabadiliko kwa kuzingatia mfano wa sauti ya lugha iliyokopa.

Hii ni mifano ya leksimu za Kiswahili ambazo zimekopwa kutoka katika lugha ya Kiingereza.

| **Leksimu mkopo** | **leksimu asili** | **Maana** | **Lugha changizi** |
|---|---|---|---|
| Bajeti | Badget | makadirio ya pesa | Kiingereza |
| Fyuzi | Fuse | kifaa cha umeme | Kiingereza |
| Fomyula | Fomula | njia ya kutenda jambo | Kiingereza |
| Rejesta | Register | Sajili | Kiingereza |

Kwa upande mwingine, lugha ya Sheng’ vilevile imeweza kuziunda leksimu zake kutoka lugha tofauti tofauti na mifano ambayo tulipata kutoka katika kazi za watafitiwa wetu ni kama vile;

| **Leksimu mkopo** | **Maana** | **Leksimu asili** | **Lugha changizi** |
|---|---|---|---|
| Mada | ua mtu | Murder | Kiingereza |
| Budee | Silaha | Bunduki | Kiswahili |
| Matime | wakati fulani | Time | Kiingereza |
| Umetrend | Umeenea | Trend | Kiingereza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Nikushow | nikuonyeshe | show | Kiingereza |
| Vibes poa | maneno mazuri | vibes | Kiingereza |
| Cheki | Ona | check | Kiingereza |
| Unaniflata | unanimaliza | flat | Kiingereza |

## 2.3 HITIMISHO

Katika sura hii tumejikita katika kuangalia mbinu mbalimbali za kuunda leksimu za Sheng'. Mbinu hizi ni pamoja na uambishaji, ukatizaji, unyambulishaji, onomatopia, upolisemia, ubunaji, akronimu, ujenzi ghairi, unyumbuzi kapa, uhulutishaji, uambatishaji, ubadilishaji silabi na ukopaji. Mbinu hizi na ambazo hutumiwa katika kuunda leksimu ambazo ni za Kiswahili pia huwa na mchango mkubwa sana katika kuuunda leksimu za lugha msimu ya Sheng'. Kutokana na ukweli huu, wanafunzi wa Kiswahili walio wa asili ya Kitachoni kutoka lokesheni ya Lwandeti hawatofautishi leksimu za Sheng' na zile za Kswahili sanifu. Hali iwapo hivi, wao hujikuta wakitumia leksimu za Sheng' katika insha zao na hata katika mazungumzo yao. Kwa hali hii, tunaweza kusema kuwa Sheng' kama lugha imechangia pakubwa matatizo ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na kisemantiki katika ufahamu wa lugha ya Kiswahili sanifu.

Katika sura ifuatayo, tunachunguza mahusiano ya fahiwa katika Sheng', lengo likiwa ni kubaini msambao uliopo wa makosa ya kisarufi katika vipengele vya mofolojia na semantiki miongoni mwa wanafunzi walio watachoni kutoka lokesheni ya Lwandeti.

## SURA YA TATU

## 3.0 MAHUSIANO YA FAHIWA KATIKA SHENG'.

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumelenga kuonyesha msambao wa makosa ambayo ni ya kimofolojia na yale ya kisemantiki kutokana na lugha kipindi ya Sheng'

Fahiwa kama wanavyoeleza Obuchi na Mukhwana (2010) ni maana inayoongezwa kwa maana msingi ya neno na huwa na uwezo wa kubadilika kwa kutegemea mazingira na wakati ambamo neno hilo limetumika.

Wanafunzi katika shule za upili wanaotumia lugha msimu ya Sheng' wanatumia fahiwa ili mawasiliano miongoni mwao iweze kufanikiwa na ni fahiwa hizi ndizo zinazoleta makosa ya kisemantiki katika matumizi ya Kiswahili sanifu wakati ambapo yanatumika kwa kutoa maana katika lugha hii kipindi ya Sheng' au maneno ya lugha msimu ya Sheng'wakati yanatumiwa katika kutolea maana katika Kiswahili ambacho ni sanifu.

Mfano wa neno 'ganji' katika Sheng' hutoa maana pia ya 'mndesha' au 'manjeka' katika kutoa maana ya neno la Kiswahili sanifu ambalo ni 'pesa'

Mifano ya maneno ya Sheng' tuliyoyapata kutoka kwa watafitiwawetu ina kiwango kikubwa cha uhusiano wa kifahiwa na maneno haya yanaweza kuingia katika uhusiano ulio wa wima kwa kuwa yanao uwezo wa kubadilishana nafasi zake katika sentensi husika na maana ya sentensi hiyo isiweze kupotea. Mifano ifuatayo ilikuwa imetumiwa na watafitiwa wetu katika insha ambazo walikuwa wameandika kwa ajili ya utafiti huu:

Ganji zimeibiwa (pesa zimeibiwa)

Njeka zimeibiwa (pesa zimeibiwa)

Katika sentensi hizi mbili hata ukibadilisha nafasi ya maneno 'njeka' na 'ganji' maana ya sentensi hizi itabakia vivyo hivyo.

Aina za Mahusiano ya kifahiwa katika lugha ni;

### 3.2 Sinonimia

Kwa mujibu wa wasemavyo Habwe na Nyonje (2010), sinonimia ni mahusiano ambayo ni ya kimaumbo katika maneno huwa maneno haya yana usawa katika lugha husika.

Mfano katika Kiswahili,

| **Neno** | **Sinonimu** |
|---|---|
| Mjinga | fala |
| Binadamu | mja |
| Kipuli | herini |
| Funga | boba |
| Beza | dharau |
| Chache | haba |

Maneno haya hudokeza na maana sawa mfano neno ‘binadamu’ lina maana sawa na neno ‘mja’

Mifano tuliyoipata kutokana na data ya utafiti wetu katika Sheng’ ni kama ifuatavyo:

| **Neno** | **Sinonimu** | **Maana** |
|---|---|---|
| Masa | Mkoro | Mama |
| Manjegee | Masanse | Askari |
| Mndesha | Ganji | Pesa |
| Soki | Ngeso | Ngumi |
| Riambez | Manzi | Msichana |
| Kurianyu | Kudedi | Kufa |
| Machali | Genge | Wanaume |

Maana katika maneno haya ni ile ile kwa mfano neno ‘masa’ na ‘mkoro’ ni maneno ambayo yana maana sawa na ‘mama’ yaani ‘mzazi wa kike.’ Maneno haya yametumika katika insha za

watafiti wetu yamejitokeza kama makosa ya kisemantiki kwa kuwa hatukupata maana inayokusudiwa katika Kiswahili sanifu.

### 3.3 Haiponimia

Habwe na Nyonje (2010) wanasema kuwa haiponimia ni uhusiano ambao huwepo baina ya maneno na hili hutokea ambapo neno moja huwa linajumuisha maana ya neno hilo au maneno mengine. Naye Wamitila (2003) anasema kuwa haiponimia hudokeza maana ambayo ni mahsusi. Hali hii pia iljitokeza katika insha za watafitiwa na kusababisha makosa ya kisemantiki na kimofolojia katika insha zao.

Mifano katika Kiswahili ni kama ifuatavyo,

| **Haiponimu** | **Haiponimia** |
|---|---|
| Ndege | Kuku, Bata. |
| Mimea | Miti, Mitunda, Maua |
| Maji | Bahari, Maziwa, Mito |
| Elimu | Msingi, Sekondari, Chuo Kikuu |
| Kazi | Udereva, Ualimu, Udaktari |

Kwa kuzingatia mifano tuliyoitoa hapo juu neno ‘Ndege’ ni haiponimu na ambayo maneno kama vile ‘Kuku’ na ‘Bata’ inachukuliwa kuwa haiponimia za neno ‘kuku.’

Lugha msimu ya Sheng’ pia inazo haiponimia kama ilivyobainika kutokana na data yetu ya utafiti.

Kwa mfano;

| **Haiponimu** | **Haiponimia** |
|---|---|
| Malesons (vipindi) | Ngoso (Kiingereza), Swa (Kiswahili, Mao (Hisabati) |
| Mawakz (kazi) | Manjege (Uaskari), Mamode (Ualimu), |
| Ganji (pesa) | Makoiro (sarafu), Marwas (noti ya mia mbili) |

Katika kuiangalia mifano ambayo tumeitoa hapo juu, mfano wa neno 'Malesons' ni neno la haiponimu kwa kumaanisha 'vipindi au ratiba' ya masomo na neno hili lina haiponimia zake nyingi zikiwemo 'Ngoso(Kiingereza)', 'Swa( Kiswahili)', na 'Mao( Hisabati )'.

**3.4 Kapitonimu**

Kapitonimu ni hali ambapo neno hubadilika kimaana herufi kubwa inapotumika mwanzoni mwa neno hilo. Mfano katika jozi ya maneno tuliyotumia hapo chini yamefanana kwa kiasi kikubwa sana kimaumbo ila utofauti hutokea tu katika kutoa maana ya neno lenyewe.

Mungu kwa maana ya 'Maulana'

mungu kwa maana ya jina la 'mmoja katika miungu mingine'

Katika lugha ya Sheng' mifano ya kapitonimu kama inavyojidhihirisha kazi za watafitiwa wetu ni kama ifuatavyo;

Fathela kwa maana ya 'Mungu' au 'Maulana'

fathela kwa maana ya 'mzazi wa kiume'

Inavyoonekana hapa ni kwamba lugha ya Sheng' pia ina mofolojia na semantiki ambayo huweza kubainika kikapitonimu. Hata hivyo, msambao wake ni mdogo ikilinganishwa na fahiwa zingine.

**3.5 Polisemia**

Wamitila (2003) anasema kuwa polisemia ni mbinu ambayo huonyesha uhusiano ambao ni wa maneno yaliyo na maana ambayo inazidi moja licha ya kuwa maneno haya yanaweza kuwa na historia ambayo ni moja.

Katika lugha ya Kiswahili mifano ni kama vile:

| **Polisemia** | **Maana** |
|---|---|
| Panda- | mgawanyiko |
| | Paji la uso |
| | Enda juu |
| | Weka mbegu ardhini |

Lugha ya Sheng' pia haijaachwa nyuma katika matumizi ya polisemia kwa mfano; data yetu ya utafiti imejitokeza na mfano huu na kudhihirisha jinsi lugha ya Sheng' inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu miongoni mwa watafitiwa wetu.

| **Polisemia** | **Maana** |
|---|---|
| Baeb | mtoto mdogo |
| | Mwanamke mpenzi |
| | Mwanamume mpenzi |

### 3.6 Antonimia

Habwe na Nyonje (2010) wanaelezea maana ya Antonimu kuwa ni yale mahusiano ambayo ni ya kimuundo pale mbapo vinyume hutokea tunapoangalia maana ya maneno mbalimbali.

Mfano ifuatayo katika lugha ya Kiswahili sanifu inasadifu;

| **Neno** | **Antonimu** |
|---|---|
| Refu | fupi |
| Tajiri | maskini |
| Eusi | eupe |
| Nene | embamba |

Lugha ya Sheng' pia haijaachwa nyuma katika matumizi ya Antonimia. Data yetu ya utafiti ilijitokeza na mifano hii na kudhihirisha jinsi lugha ya Sheng' inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu miongoni mwa watafitiwa wetu.

| **Neno** | **Antonimu** |
|---|---|
| Omoka (tajirika) | sota (maskini) |
| Pasi (kupita) | dunda (kuanguka) |
| Mng'aro (mpya) | chapa (zeeka) |
| Inabamba (inapendeza) | inaboo (inaudhi) |

Mtoi (mtoto)                                    mzae (mzee)

Amechoma (ameharibu)                    ameweza (amefaulu)

Maneno haya tuliyotolea mifano hapo juu yanaonyesha kuwa yana mahusiano ya kiantonimia na kwamba hupatikana pia katika lugha ya Sheng' na kusababisha athari za ujifunzaji mbaya wa Kiswahili sanifu.

**3.7 HITIMISHO**

Katika hii sura tumechunguza mahusiano ya fahiwa katika Sheng' lengo letu likiwa ni kubaini msambao uliopo wa makosa ya kisarufi katika vipengele vya mofolojia na semantiki katika watafitiwa wetu ambao ni wanafunzi wa sekondari na ambao ni wenye asili ya Kitachoni. Tumezingatia uhusiano wa kifahiwa katika leksimu ambazo ni za Sheng'. Vifahiwa hivi vinapotumiwa katika lugha ya Kiswahili huwa vinasababisha utata ambao huchangia makosa katika maana hivyo kuzua makosa ambayo ni ya kisemantiki na kimofolojia katika lugha ya Kiswahili haswa kupitia maandishi ya wanafunzi jinsi imedhihirika katika insha ambazo tuliwapa watafitiwa wetu hivyo kusababisha matokeo duni katika mitihani ya wanafunzi hawa kwa Kiswahili haswa katika mtihani wa kitaifa wa Karatasi la Kwanza na Karatasi la Pili wa kidato cha nne unaofanywa mwishoni mwa mwaka wa nne. Makosa ambayo wameyafanya katika kuzingatia haiponimia, sinonimia, homonimia, polisemia na antonimia tutayajadili kwa kina katika sura ya nne haswa kwa kutumia mifano ambayo wametumia wanafunzi wa sekondari katika kidato cha kwanza, kidato cha pili, kidato cha tatu na kidato cha nne katika shule ambazo tumeteua

# SURA YA NNE

## 4.0 MAKOSA KATIKA KAZI ZA WANAFUNZI.

### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii ya nne, tumechunguza makosa tofauti tofauti ambayo wanafunzi walio Watachoni wameyafanya katika kazi zao za insha katika shule za upili tatu ambazo ni shule ya upili ya Maturu, shule ya upili ya Lwandeti D.E.B na shule ya upili ya Lukhokho. Hizi ni shule ambazo hupatikana katika lokesheni ya Lwandeti kutoka kaunti ya Kakamega. Tumechunguza vyanzo vya makosa ya wanafunzi hawa na kisha tukawapa njia mwafaka za kusuluhisha makosa hayo haswa yanayotokana na athari za Sheng' ili wasirudie makosa yale katika kazi zao za uandishi. Madhumuni ya utafiti huu wetu ilikuwa ni kuchunguza kama kweli lugha ya kipindi ya Sheng' husababisha makosa ya kimofolojia na pia ya kisemantiki katika uandishi wa wanafunzi wa shule za upili na kama wanavyodai Swan na Smith (1987) wanaodai eti lugha mbili zikiingiliana basi ndivyo makosa hutokea na ndiposa tukaonelea kuwa nadharia ya lugha kadirifu itatuelekeza katika kubaini makosa haya ambayo ni ya Kimofolojia na yale ya Kisemantiki ambayo wanafunzi wanayafanya katika kazi zao.

Makosa ambayo yamefanywa na wanafunzi ni kama ifuatavyo:

### 4.2. Makosa ya Kimofolojia

Ukiukaji wa kanuni mbalimbali za kuunda maneno husababisha kutokea kwa makosa ya kimofolojia. Makosa haya ya kimofolojia yanaweza kujitokeza ama katika neno zima au katika mofu za neno hilo tu. Leksimu za lugha kipindi ya Sheng' mara nyingi zimejumuishwa katika lugha sanifu ya Kiswahili hivyo miundo ya maneno hayo inaathiriwa na ni jambo ambalo husababisha kuwepo kwa makosa ambayo ni ya kimofolojia.

Mifano ni kama ifuatavyo;

#### 4.2.1. Ukopaji.

Katika utafiti huu tumebaini kuwa wanafunzi wengi wanatumia leksimu za lugha nyingine haswa za Sheng' katika kuwasiliana kwao na pia katika maandishi yao. Pia, wanafunzi hawa wanatumia

maneno ambayo wanayakopa moja kwa moja kutoka Sheng' na kuyaswahilisha baada ya kuyafanyia maneno hayo mabadiliko machache.

Kwa mfano:

1. Mode anakam daro. (Mwalimu anakuja darasani)

2. Fathe kuna madaeizi haonekani. (Kuna siku kadhaa baba hajaonekana).

3. Mie ni msik. (Mimi ni mgonjwa).

4. Karibu matha kanairoo utatrend mbaya (karibu mama Nairobi sifa zako zitaenea.)

5. Manze huyu dame ananiflata mbaya (kweli huyu msichana amenivutia sana)

Maneno kama Madeiz (days) na Msik (sick), Matha (mother) na flata (flat) kama yanavyojitokeza katika kazi za watafitiwa wetu yamekopwa kutoka katika lugha ya Kiingereza na kutumiwa katika lugha ya Sheng' ilhali maneno kama vile 'Daro' (Darasa) na mie (mimi) yamekopwa kutoka lugha ya Kiswahili na kisha yakafanyiwa mabadiliko ya ukatizaji tamati.

Miundo ya maneno katika lugha changizi na lugha pokezi huwa zinafanana.

**4.2.2. Ubunaji**

Hii ni mbinu ambapo maneno huwa yanabuniwa kutoka lugha ya kwanza (changizi) na kutumiwa katika lugha ya pili (pokezi). Makosa ya kimofolojia hutokea pale ambapo maneno ya lugha ya kwanza yanatumiwa katika lugha ya pili.

Mbinu hii ya ubunaji hutumika katika lugha ya Kiswahili na ile ya Sheng' katika kujiundia leksemu zake hivyo maneno ambayo ni ya Sheng' yanapotumiwa katika maandishi ya Kiswahili sanifu huwa inasababisha makosa ya kimofolojia. Data ya utafiti wetu ilijitokeza na mifano ifuatayo;

1. Masa alikuwa atupe ganji moro. (Mama alikuwa atupe pesa kesho.)

2. Niliwasho tujitoe. (Niliwaambia tuondoke.)

3. Mazee kiasi tu nakam. (Jamani nisubiri kidogo nakuja.)

4. Kigonyi wa mat ametuweka hapa sana (kondakta wa matatu ametuchelesha sana)

5. Nipo kejani nina doz (Nipo chumbani mwangu nalala)

6. Mboch wetu ananiboh sana (Simpendi mfanyikazi wetu wa nyumba )

Maneno ya Sheng’ kama vile ‘masa’,’tujikate’,’ganji’,’mazee’,’nakam’ na kadhalika hutumika na wazungumzaji wa lugha ya Sheng’ na husababisha makosa ya kimofolojia yanapotumiwa kwa Kiswahili sanifu.

### 4.2.3. Uambishaji

Hii ni mbinu ya kupachika viambishi katika mizizi ya maneno. Uambishaji umechangia pakubwa kuzua makosa ambayo ni ya kimofolojia miongoni mwa kazi za wanafunzi. Katika hali hii, viambishi awali au viambishi tamati huongezwa katika maneno yale. Vivyo hivyo, lugha ya Sheng’ hutumia mbinu hii kama ilivyojidhihirisha kutokana na data ya utafiti wetu.

Hivi ndivyo lugha ya Sheng’ ilionekana ikiathiri Kiswahili miongoni mwa watafitiwa kimofolojia.

1. Mabeste wangu walinipa tuganji. (Marafiki zangu walinipa vijipesa au pesa kidogo) Katika mfano huu, mofimu {ma} katika neno’ mabaste’ imewakilisha wingi wa wahusika na mofimu (tu) katika neno ‘tuganji’ inaashiria udogo au udunishaji.
2. Karibu Kanairo mji wa mabazuu. (Karibuni Nairobi mji wa wazee) mfano huu mofimu (ka) katika neno ‘Kanairoo’ yaani Nairobi linaonyesha udunishajo au udogo.

### 4.2.4. Upolisemia

Katika kuchunguza mbinu ya Upolisemia, maneno mengi yaliyokopwa kutoka lugha nyingine hufanyiwa upanuzi ili yapate maana mpya.

Data yetu ya utafiti ilitupa mifano ifuatayo;

1.Alikuwa msupuu kuruka. (Anavutia sana).

2. Alituwishia vipoa kwa exams. (Alitutakia mema kwa mitihani).

Katika mifano iliyopo hapo juu, watafitiwa wametumia mbinu hii ya upolisemia katika maneno mfano katika: ’kuruka‘na ‘vipoa’, neno ‘vipoa’ limepanuliwa kwani limetokana na neno “poa” kwa maana ya ‘kuwa baridi’ katika lugha sanifu ya Kiswahili ilhali katika muktadha wa Sheng’ ni ‘vizuri sana’ nalo neno ‘kuruka’, katika Sheng’ linaashiria, ”kupita kiasi”, ila katika Kiswahili

sanifu neno hili linamaanisha kitendo cha mtu kuinuka na kwenda juu hewani kwa kutumia miguu yake. Pia neno ‘msupuu’ lina maana ya mrembo au msichana ambaye ana muonekano mzuri ilhali neno hili katika Kiswahili humaanisha ‘mchuzi’. Hivyo, maneno haya ya upolisemia yanapotumika katika lugha sanifu ya Kiswahili huwa yanazua makosa tofauti tofauti ya kimofolojia na kisemantiki kama ilivyojidhirisha katika insha za watafitiwa wetu.

Wanafunzi walio Watachoni kutoka katika Lokesheni ya Lwandeti huwa wanayafanya makosa haya ya kimofolojia na kisemantiki kwa sababu zao ambazo ni pamoja na uzoefu wa kuitumia lugha hii ya Sheng’ katika mawasiliano yao nyumbani au hata shuleni.

Pili, wanafunzi wengine huyafanya makosa haya kwa kutojua ni yapi maneno ya Sheng’ na ni yapi haswa ya Kiswahili sanifu hivyo ni kwa mapuuza tu.

Tatu, kuna wale hukosa kabisa msamiati wa Kiswahili sanifu hivyo kulazimika kutumia lugha iliyo ya Sheng’ ili kutimiza mahitaji ya mawasiliano yao na mwisho, wanafunzi wengine husahau mazingira au muktadha wa matumizi ya lugha hizi mbili ahta hivyo ni wazi kuwa wengi wa wanfunzi hawa hutumia lugha hii ya Sheng’ ili kuondoa ukinaifu wa kutumia lugha sanifu ya Kiswahili Shuleni.

Makosa ambayo yalifanywa na watafitiwa wetu na ambayo ni ya kimofolijia tulihakikisha tumeyachanganua kwa kutumia takwimu na kubaini ni kiwango gani cha asilimia makosa haya yalikuwa nazo ili tuweze kutambua ni wanafunzi kutoka vidato vipi ambao huwa wanaathirika pakubwa na lugha hii ya Sheng’ katika shule hizi tulizokuwa tunatafiti na ambazo ni shule ya upili ya Maturu, shule ya upili ya Lukhokho na ile ya Lwandeti D.E.B. Katika kuyachanganua makosa ambayo wanafunzi hawa walikuwa wameyafanya na tuliweza kuanza kwa kuyahesabu makosa ambayowanafunzi hawa waliyafanya kutoka vidato mbalimbali walikuwa wamefanya na kisha baadaye tukayaweka pamoja makosa haya ya kimofolojia kwa kuyajumuisha na mwishowe tulitathmini idadi halisi ya asilimia ya makosa ya kimofolojia katika kila kidato vifuatavyo;

Jumla ya makosa ambayo ni ya kimofolojia yaliyofanywa na watafitiwa wetu ni 730

| **Kidato** | **Makosa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Kidato cha nne | 250 | 34.2% |
| Kidato cha tatu | 202 | 27.7% |

| | | |
|---|---|---|
| Kidato cha pili | 140 | 19.2% |
| Kidato cha kwanza | 138 | 18.9% |

Matokeo haya yalibaini kuwa wanafunzi wanaosoma katika vidato ambavyo ni vya kiwango cha juu; yaani wale wa kidato cha tatu na nne; ndio walionekana wameathirika kwa asilimia za juu katika kuitumia lugha hii ya Sheng' katika maandishi yao kwani tulipata asilimia 34.2% katika kidato cha nne ilihali cha tatu kikiwa na asilimia 27.7% ikilinganishwa na wale wa vidato vya chini yaani wa kidato cha pili na kidato cha kwanzo. Matokeo haya yanadhihirisha wazi kuwa wanafunzi wengi huathiriwa zaidi na lugha hii pindi wanapoendelea kukaa katika mazingira ya sshuleni. Wengi wanabainika kutumia lugha hii katika kuficha usiri miongoni mwao, wengine wanaitumia ili kujinasibisha na makundi mengine ya wanafunzi haswa wanaotoka mijini haswa walio karibu na mji wa Webuye.

### 4.3 Makosa ya Kisemantiki

Makosa ya kisemantiki hudokeza athari katika maana katika maneno fulani, virai na sentensi kwa ujumla. Hapa iwapo neno likipata athari ya maana katika sentensi huwa maana hiyo imeaithiri sentensi yote kwa ujumla basi kuifanya sentensi hiyo kubadilika kimaana. Utafiti wetu umebaini kuwa maana ya maneno mengi huwa inabadilika kutokana na kuwepo kwa uhusiano wa upolisemia ambapo hudokeza kuwepo wa maana zaidi ya moja katika maneno. Hili ni suala ambalo limezua utata katika kufasiri maana na kusababisha makosa ambayo ni ya kisemantiki kutokea.Wanafunzi wa shule za sekondari katika lokesheni ya Lwandeti wamefanya makosa haya haswa katika maandishi ya insha zao. Mifano ifuatayo ilijidhihirisha katika kazi za watafitiwa wetu;

1. Afta kumada niliwasho mabeste wa mine tujikate. (Baada ya kumaliza niliwaambia rafiki zangu tuondoke).
2. Tulishtuka juu tulijua mhadhara umetuget. (Wasiwasi ulituingia kwa kuwa tulijua tumepatwa na matatizo).
3. Demu wake ni msupuu kuruka. (Mpenzi wake anavutia kweli).
4. Doo zake zilikuwa finje. (Pesa zake zilikuwa hamsini).

Maneno ambayo ni ya kukopwa kutoka katika Kiswahili yanapotumiwa katika lugha ya Sheng' huwa yanakuwa na fahiwa tofauti kabisa. Mifano ambayo tumetumia hapo juu neno'tujikate'

katika Kiswahili sanifu lina maana ya kutumia kifaa chenye makali kutenganisha kitu katika vipandevipande ilihali katika muktadha ambamo neno hili la Sheng' limetumiwa lina maana ya kwenda au kuondoka. Na kutokana na sababu hii, neno hili 'tujikate' hupoteza maana yake ya kisemantiki wakati wa kutumika kwalo katika Kiswahili sanifu. Katika mfano wa pili neno 'mhadhara' lina maana ya 'matatizo au shida' fulani ambayo imewapata wahusika hawa ilihali katika lugha sanifu ya Kiswahili mhadhara ni mafunzo ya chuo kikuu, hivyo pia kisemantiki maana ya neno hili limepotoshwa.

Kwa kuangalia kazi za watafitiwa wetu katika vidato mbalimbali, tumeweza kubainisha makosa ya kisemantiki ambayo watafitiwa hawa wameyafanya na kubainisha ni kwa asilimia ngapi wameathirika katika kuyatumia makosa haya.

Nayo ni pamoja na:

Idadi ya makosa ya makosa ya kisemantiki kwa jumla = 320.

| **Kidato** | **Idadi ya makosa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Nne | 130 | 40.6% |
| Tatu | 100 | 31.3% |
| Pili | 60 | 18.8% |
| Kwanza | 30 | 9.4% |

Katika kuangazia kiwango cha kisemantiki, wanafunzi walio katika kidato cha nne hasa walionekana kuwa wameathirika zaidi tukilinganisha na wale wa vidato vya chini yaani kidato cha kwanza, pili na cha tatu licha ya kuwa nao pia waliathirika ila ni kwa asilimiaya chini. Ni wazi kuwa muda unavyoendelea kusonga, wanafunzi hawa wakiwa shuleni na kutangamana na wanafunzi wenzao ndivyo wanavyo imarika zaidi katika matumizi ya lugha hii msimu ya Sheng' na ndiposa wakaonyesha kuathirika pakubwa katika uandishi wao wa insha katika makosa ya kisemantiki ambayo yanatokana na lugha ya Sheng'.

Matokeo ya utafiti wetu imebaini kuwa wengi wa wanafunzi hufanya makosa ya kimofolojia kwa asilimia ya juu tukilinganisha na makosa ambayo ni ya kisemantiki katika insha walizoandika. Baada ya kupata kuona msambao wa makosa ya kimofolojia na kisemantiki

yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili wa asilia ya Kitachoni, na hata kudhihirisha vianzo vya makosa haya, hebu sasa tutie mikakati ya kuzuia makosa haya katika kisehemu kifuatacho:

### 4.4 Mikakati ya Kuzuia Makosa Yatokanayo na Sheng'.

Sheng' kama lugha kipindi ya Kiswahili inatumika na wanafunzi, walimu wafanyikazi wa shule na hata wazazi. Ni kutokana na hali hii ambapo imepanuka sana katika matumizi yake. Hivyo basi kuna baadhi ya mbinu ambazo tumeonelea kuwa zitatusaidia sana sisi kama watafiti kuhakikisha kuwa lugha hii imefishwa kabisa miongoni mwa wanafunzi na kuhakikisha kuwa wanatia fora katika utumizi wa Kiswahili sanifu. Tumekuwa na mazungumzo na walimu wa shule za upili wa Kiswahili sanifu katika shule ambazo tumetafiti na kwa pamoja wakatoa maoni yao na ambayo kwetu ndiyo mikakati ya kukabili matumizi ya Sheng' katika insha za wanafunzi.

**Mbinu au mikakati hii ni pamoja na:**

#### 4.4.1 Kupigia Mstari Maneno au Sentensi zenye Makosa.

Katika kusoma kazi ambazo zimeandikwa na wanafunzi hawa, tumekuwa tukiyapigia makosa ambayo mwanafunzi amefanya mistari na kuandika majibu sahihi juu ya neno ambalo lina makosa kwa kutumia kalamu nyekundu ili mwanafunzi huyu aweze kubaini makosa ambayo amefanya ili asiweze kuyarudia tena makosa haya wakati anapoandika insha nyingine au kazi yoyote ile ya Kiswahili .

#### 4.4.2 Kusisitiza Nafasi na Umuhimu wa Kiswahili Sanifu.

Pana haja kubwa ya kusisitiza matumizi ya Kiswahili ambacho ni sanifu katika shule za upili kwani Kiswahili ndiyo lugha ambayo hutumika katika utahini wa mitihani ya Kiswahili katika karatasi la kwanza, la pili na la tatu katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne na wale wanafunzi wanaoitumia lugha ya Sheng' katika maandishi yao wanafaa kutuzwa alama chache ikilinganishwa na wale wanaoitumia lugha sanifu na ambao wanafaa kutuzwa alama za juu na pia kusifiwa na mwalimu wao au hata kuzawidiwa darasani ili wanafunzi wengine wawe na mtazamo hasi kuihusu matumizi ya lugha hii ya Sheng' shuleni. Walimu pia wasisitize umuhimu wa wanafunzi kutumia lugha sanifu shuleni hasa katika gwaride na katika vipindi vya Kiswahili darasani.

#### 4.4.3 Kuweka Mabango Yanayokejeli Matumizi ya Sheng'.

Walimu na wanafunzi wahakikishe kuwa wameyaweka mabango kwenye sehemu mbalimbali zilizo wazi ili kuhakikisha kuwa wanapinga matumizi ya lugha hii msimu ya Sheng'. Mifano ya maneno ya Sheng' iandikwe katika mabango na maana za maneno haya katika Kiswahili sanifu zibainishwe kwa herufi kubwa zinazosomeka kwa urahisi na yawekwe katika sehemu kama vile kwenye lango kuu la shule mbele ya madarasa, vyumba vya maanguli na kadhalika. Haswa sehemu zozote ambapo wanafunzi wanaweza kusoma kwa urahisi ili waepuke makosa haya katika maandishi yao.

#### 4.4.4 Walimu Washiriki Mazungumzo na Wanafunzi.

Walimu wana mchango mkubwa sana katika kuhakikisha kuwa wanafunzi hawatumii lugha hii ya Sheng' katika mazingira ya shuleni na wanapowasiliana na katika uandishi wa kazi zao.Walimu wahakikishe kuwa wamefundisha wanafunzi wote athari za lugha hii msimu ya Sheng' darasani kwani ni chanzo cha wao kufeli katika mtihani wao wa kitaifa. Pia, walimu hawa wawape kazi au insha wanafunzi na wasahihishe kazi hiyo kwa kuonyesha wanafunzi makosa ambayo yanatokana na Sheng'. Kupitia marekekebisho haya wanafunzi wengi wataanza kuepuka matumizi ya lugha hii ya Sheng' katika mawasiliano yao na pia katika kazi zao za uandishi.

#### 4.4.5. Kuwaita Wanafunzi na Kuwarekebisha Papo Hapo.

Makosa yafanywayo na wanafunzi yaweze kurekebishwa papo hapo na walimu. Viranja pia wawe katika mstari wa mbele kusaidiana na walimu kutambua wanafunzi wanaotumia lugha hii ya Sheng' katika maongezi yao, walimu wawaite wanafunzi huwa na kuwarekebisha mbele ya wanafunzi wenzake hasa darasani au kwenyw gwaride hivyo wanafunzi hawa wataweza kujua kuwa si vyema kutumia lugha hii ya Sheng' kwa namna yoyote ile katika mazingira ya shuleni. Pia, insha za wanafunzi walioathirika na lugha hii msimu ya Sheng' ziweze kusomwa mbele ya darasa ili wanafunzi wengine watambue makosa yanayotokana na athari za Sheng' ya kimofolojia na kisemantiki. Hivyo itakuwa ni njia rahisi ya kuyarekebisha makosa haya.

### 4.4.6. Marufuku Kwa Filamu na Majarida Yanayotumia Lugha ya Sheng'

Wanafunzi haswa wanaosomea shule za bweni huwa na muda wa burudani na ilibainika kuwa wengi hutumia filamu zilizosheheni matumizi ya Sheng' mfano za 'DJ AFRO' na ni vyema filamu za aina hii zipigwe marufuku shuleni ili wanafunzi waweze kutumia filamu zinazotumia lugha sanifu shuleni. Pia, majarida yanayosomwa na wanafunzi yawe ni yale yanatumia Kiswahili sanifu na mfano wa jarida la Shujaz ambalo ni maarufu sana miongoni mwa vijana na ambalo limeandikwa kwa lugha ya Sheng' liwe marufuku kwa wanafunzi wa shule za upili.

### 4.4.7. Walimu Wawe Vielelezo Vyema kwa Wanafunzi.

Walimu wawe katika mstari wa mbele katika kutumia Kiswahili sanifu ndani na nje ya mazingira ya darasani ili wawe mfano mwema kwa wanafunzi kwa kuwa imebainika kuwa wengi wa wanafunzi huwaiga walimu wao wanapozungumza.

## 4.5 HITIMISHO

Katika hii sura ni wazi kuwa wanafunzi wengi walio katika shule za upili huyafanya makosa ambayo ni mengi sana ya kimofolojia na ya kisemantiki kutokana na uzoefu wao wa kuitumia lugha msimu ya Sheng' katika mawasiliano yao ya kila siku. Makosa haya ambayo yameathiri wanafunzi walio Watachoni katika mitihani yao ya kitaifa haswa katika mtihani wa Kiswahili kwani tumebaini kuwa kumekuwepo na msambao wa lugha hii kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne na katika utafiti huu wetu tumebaini kuwa wanafunzi wanapoingia katika kidato cha kwanza, wengi huwa hawajaathirika pakubwa na lugha hii kipindi ya Sheng', lakini pindi tu wanapoingiliana na wanafunzi walio wa vidato vya juu huwa wanaimarika zaidi katika kuitumia lugha hii katika muktadha wa shuleni jambo ambalo husababisha wanafunzi wa kidato cha nne kuwa ndio wenye kuathirika pakubwa kwa asilimia ya juu zaidi jinsi ilivyodhihirika katika utafiti wetu miongoni mwa watafitiwa walio Watachoni tukiwalinganisha na wale wa vidato vya chini. Walimu pia wameonekana kuwa miongoni mwa wanaoendeleza lugha hii ya Sheng' shuleni kwa kushiriki mazungumzo na walimu wenzao au hata wafanyikazi wa shule kwa kutumia lugha msimu ya Sheng' ila tumependekeza adhabu kali ichukuliwe kwa wanafunza wanaoonekana na kusikika wakiitumia lugha ya Sheng' hadharani katika mawasiliano katika mazingira ya shuleni hivyo kuchangia pia kwa wanafunzi kuathirika katika maandishi yao. Ni

wazi kuwa makosa haya yanayotokana na athari za Sheng’ husababishwa na mbinu zikiwemo ukopaji, ukatizaji na ubunaji na pia mahusiano yaliyo ya upolisemia. Katika kuhakikisha kuwa lugha hii msimu haitumiwi tena shuleni, tumependekeza mikakati mbalimbali ya kutumia ikiwemo mwalimu kupigia mstari maneno yaliyo na makosa, kurekibisha makosa hayo kwa kuandika majibu ambayo ni sahihi juu ya maneno yaliyo na makosa na pia, walimu na viranja wote kwa ujumla wasisitize kuwa lugha iliyo sanifu pekee ndiyo inafaa kutumiwa katika mazingira ya shuleni na pia mabango mbalimbali yawekwe shuleni yanayopinga matumizi ya lugha ya Sheng’ shuleni na mabango haya yawekwe sehemu ambazo ni wazi ili kuhakikisha kwamba wanafunzi hawataitumia tena. Hivyo pia pawepo na mazungumzo ya kina miongoni mwa walimu na wanafunzi kuhusu matumizi ya lugha hii na athari zake kwa wanafunzi haswa katika vipindi vya Kiswahili darasani.

## SURA YA TANO

## 5.0. MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO.

### 5.1 Muhtasari.

Utafiti huu umekuwa na malengo matatu ambayo yamekuwa kuchunguza ni kwa kiasi gani Sheng’ husababisha matatizo ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na ya kisemantiki miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wanaozungumza Kitachoni kama lugha yao ya kwanza , pili, kubaini msambao wa makosa ya kisarufi katika vipengele vya mofolojia na semantiki uliopo kutokana na Sheng’ miongoni mwa wanafunzi Watachoni katika vidato mbali mbali na tatu; kudhihirisha vyanzo vya makosa ya kisarufi yaliyo ya kimofolojia na kisemantiki yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili walio Watachoni.

Sheng’ kama lugha kipindi ya Kiswahili imeenea sana katika matumizi yake miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili na hivyo imekuwa na athari hasi miongoni mwa wanafunzi hawa ni suala ambalo limepelekea wanafunzi wengi kufeli katika mitihani yao ya kitaifa hasa ikikumbukwa kwamba Kiswahili ni somo ambalo ni la lazima katika shule za upili na hutahiniwa mwishoni mwa mwaka wa nne katika mtihani wa kitaifa katika shule za upili.

Katika sura ya pili, tumechunguza mbinu mbalimbali za uundaji wa leksimu za Sheng’ ambazo ni pamoja na onomatopia, uambishaji, ukopaji, ukatizaji, uambatishaji upolisemia, ubadilishaji silabi, ubunaji, akronimu, uhulutishaji na unyambulishaji.

Tumechunguza pia jinsi leksemu hizi zinavyoundwa hali inayopelekea makosa mengi ya kimofolojia na yale ya kisemanti kina kuendelea kuwepo katika Kiswahili hasa katika kitengo cha uandishi wa insha.

Katika sura ya tatu, tumeangazia ni kwa namna gani wanajamii hutumia vifahiwa kadha wa kadha katika lugha ya Sheng’ kuvipa Sheng’ maana. Mahusiano ya fahiwa tuliyotalii ni kama vile: Antonimia, Kapitonimu, Haiponimia, Polisemia na Sinonimia. Imebainika kwa wazi kuwa vifahiwa hivi ndivyo ambavyo husababisha utata hasa wa maana wakati vimetumika katika lugha ya Kiswahili sanifu. Jambo hili husababisha maana katika maneno au katika sentensi kupotea na hivyo kuzua makosa ya kisemantiki na kwa hivyo kupelekea wanafunzi wa asili ya Kitachoni kufeli katika mitihani yao ya Kiswahili katika mitihani ya kitaifa.

Nayo sura ya nne imeangazia makosa mbalimbali ambayo ni ya kimofolojia na yale ya kisemantiki katika kazi za wanafunzi walio Watachoni katika kijiji cha Lwandeti. Kupitia utafiti wetu, tumebaini kuwa wanafunzi walio watachoni huathiriwa na matumizi ya lugha hii ya Sheng' haswa wale ambao wapo kwenye vidato vya juu ambavyo ni kidato cha tatu na kile cha nne.Wanafunzi hawa hutumia lugha msimu ya Sheng' kwa mawasiliano yao hivyo wameimarika zaidi ukilinganisha na wale wa vidato vya chini ambavyo ni kidato cha kwanza na cha pili.

**5.2 Mahitimisho.**

Utafiti huu wetu ulikuwa unaangazia athari za lugha kipindi ya Sheng' miongoni mwa wanafunzi wa sekondari katika shule za lokesheni ya Lwandeti zikiwemo shule ya upili ya Maturu, Lwandeti D.E.B na ile ya Lukhokho. Kwa kutumia nadharia **y**a lugha kadirifu ambayo iliasisiwa na Selinker (1969), tumeweza kuyachanganua makosa ambayo yamefanywa na watafitiwa wetu kwa kuzingatia kigezo cha kimofolojia na kile cha kisemantiki.Tumebaini kuwa wanafunzi wa shule za upili walio Watachoni hutumia Sheng' katika vidato vyote licha ya kubaini kwamba wale wa vidato vya juu ndio walioathirika kwa asilimia ya juu kutokana na kuwa hawa wameimarika katika kuitumia lugha hii. Pia, ni wazi kwamba wanafunzi wengine imebainika kuwaiga walimu wao ambao hutumia lugha ya Sheng' shuleni jambo ambalo limekuwa gumu kuwaelekeza wanafunzi wao kuepuka kutitumia lugha hii ya Sheng'. Malengo ya utafiti wetu pia yameshughulikiwa ipasavyo kwa kuwa tumetambua vyanzo mbalimbali vya makosa waliyofanya na wanafunzi na namna ya kuyarekebisha makosa haya.Wanafunzi wa Kiswahili walio Watachoni wanatumia baadhi ya leksimu ambazo ni za Sheng' katika Kiswahili sanifu na kuathiri matokeo yao ya mitihani ya kitaifa ambayo huwa duni. Nadharia ambayo imetuelekeza katika kufafanua makosa wanayoyafanya wanafunzi hawa na ambayo ni ya lugha kadirifu imetusaidia kwani tulijikita katika mihimili yake yote na hivyo ikatufaa pakubwa kutambua makosa ambayo wanafunzi hawa wamefanya katika kujifunza lugha iliyo ya pili. Makosa haya ya kimofolojia na ndio yanayowasababishia kufeli katika mitihani yao katika Kiswahili na hasa katika uandishi katika Karatasi la Kwanza na na la Pili haswa kuhusiana na sehemu ya sarufi na matumizi ya lugha licha ya kuwa karatasi hili husahihishwa kwa umakinifu mkubwa kwa kuwaadhibu watahiniwa kwa makosa ya sarufi na yale ya hijai wanayoyafanya na kwa hivyo kusababisha wapate alama za chini kabisa katika mitihani yao.

**5.3 Mapendekezo.**

Katika utafiti huu tumekuwa tukitathmini athari za lugha kipindi ya Sheng' kwa wanafunzi wa Kiswahili walio Watachoni kutoka lokesheni ya Lwandeti. Ni wazi kuwa lugha hii imewaathiri kwa kiwango kikubwa wanafunzi kutokana na matokeo duni ambayo wanafunzi hawa hupata katika mitihani yao ya kitaifa ya kidato cha nne.Utafiti huu wetu ulijikita hasa katika kuangalia ni kwa vipi wanafunzi hawa wanaathirika na ni mapendekezo yetu kuwa tafiti nyingi zifanywe ili kubaini vyanzo zaidi, kwa kuwa hata wazazi, walimu na wadau wengine wasio wasomi wameathirika na lugha hii ya Sheng'. Ili kuondoa matatizo ya athari hizi za Sheng' tunapendekeza tafiti nyingine zifanywe. Tafiti hizi zinaweza kuhusisha vipengele vyote vya muundo wa lugha ya Kiswahili vilivyo vya fonolojia, mofolojia, sintaksia,na semantiki kwa namna vinavyoathirika kutokana na Sheng'.

Pili, mchango wa wazazi pamoja na wadau wengine uweze kutathminiwa kwa namna ambavyo unaathiri Kiswahili kutokana na athari hasi za Sheng'

Tatu,suala la jinsia na matumizi ya Sheng'dhidi ya Kiswahili sanifu liweze kutafitiwa kwa namna linavyoathiri wanafunzi wa sekondari katika ujifunzaji wao wa lugha ya Kiswahili sanifu na athari zake katika mtihani wa kitaifa.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M. H na Osinde, K. (1997). *'Sheng' and English in Nairobi. Development of mixed codes among the urban youth in Kenya.'* International journal of Sociology of Language. 125:43-65.

Akoth, B. (2015*). Uchanganuzi Makosa na Muundo sentensi: Ulinganisho wa sentensi sahili za Kiswahili na Kisuba.* Tasnifu za Uzamili ambayo bado haijachapishwa CHUO KIKUU CHA NAIROBI

Amanda, L. (2011). *'Pohamba's Namlish Offers Light Relief.' The Namibian.* August 12.

Bosire, M. (2008). *Sheng'. The Phonological, Morphological and Social Profile of an Urban Vernacular*.Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa: University of Albany. State University of New York.

Buliba, A. Njogu, K. na Mwihaki, A (2006). *Isimu jamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili.* Nairobi. Jomo Kenyata Foundation.

Briton, L. J (2000). *The Structure of Modern English. Alinguistic Intro Illustrated Edition.* John Benjamin Publishing Company.

Corder S. P. (1967). *Error Analysis and Interlanguage.* Oxford. Oxford University Press.

Corder. S. P. (1981) *Error Analysis*. London. Longman Publishers

Echessa, P.G. (1990). *A Study of the Word Structure and processes involved in Word Formation in Sheng'.* A Case study of Eastlands area in Nairobi. Tasnifu ambayo haijachapishwa.

Gass, S. na Selinker, L. (2008) *Second Language Acquisition: An Introductory Course.* New York. Routledge.

Githinji, P. (2008*). Language Attitudes: Nairobi Peoples and Sheng*. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa, Michigan State University.

Githiora, J. (2002). *'Sheng': Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole?'* Journal of African cultural Studies. University of London vol. 15 pp159-183

Hartman R. K. na F.C. Stork, (1972). *Dictionary of Language and Liguistics*. London: Applied Science Publishers Ltd.

Hudson, R. A. (1996). *Sociolinguistics*, (2nd Edition) Combribge, C.U.P.

Iribemwangi, P.I.& A. Mukhwana, (2011) *Isimujamii*. Nairobi. Focus Publishers Ltd.

Kachipela, D. (2014). *Athari za Sheng' katika Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili katika shule za Msingi mtaa wa Kangemi.* Tasnifu ya uzamili ambayo bado kuchapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi.

Katie, W. (2001*). A Dictionary of Stylistic*. Longman: Halow.

Larsen, M. H. (1992). *An Introduction to Language Two Acquisition Research*. Longman. London

Mahu, F. (2009) *'Leave Sheng' to Matatu Touts and Musicians.* The Standard, September 29

Mazrui, A.M. (1995). *"Sheng' and Code Switching: The Case of Sheng' in Kenya*." Africanistich Arbeitspapier 41: 168-179

Mbaabu, I. na K. Nzuga, (2003). *Sheng'- English Dictionary:* Deciphering East Africa's Underworld Language. Dar es Salaam: TUKI.

Mekonge, L. (2016). *Athari za Sheng'katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili za Gusii.* Tasnifu ya uzamili ambayo bado kuchapishwa.

Momany, C. (2009*). "The Effects of Sheng' in the Teaching of Kiswahili in Kenyan Schools."* The Journal of Pan African Studies.

Njoroge, F. (2014). *Hali, hadhi na majukumu ya Sheng' mjini Nakuru.* Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi

0gechi. N. O. (2002). *Code Switching in Kenya Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng*.Tansifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Hamburg: University of Hamburg.

Ogechi, N. O. (2005): *Lexicolization in Sheng'.* Nordic Journal of African Studies 14(3), 334-355.

Okoto, W. L. (2015). *Athari za Sheng' kwa lugha ya Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haichachapishwa.

Osinde, K. (1987). *Sheng': An investigation into the Social and Structural Aspects of An Evolving Language.* Tasnifu ya B. A. ambayo bado haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sabiti, B. (2015) '*One of the Funniest and Strangest English Varieties in the World.'* Daily Monitors, February 20.

Selinker, L. (1969) *Language transfer. General linguistics.* New York. Rawlence Eribaum Associates.

Selinker, L. (1972) *Interlanguage.* New York. Rawlence. Eribaum Associate

Swan, M. & Smith, B. (1987) *Learners English: Ateacher's Guide to Inteference and other Problem.*Cambridge . Cambridge University Press.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi na Nadharia.* Nairobi . Focus Books.

**KIAMBATISHO A – MAHOJIANO.**

**<u>Mahojiano baina ya mtafiti (Rehema) na walimu wa shule za upili za Maturu, Lwandeti D.E.B. na Lukhokho.</u>**

(Mimi ni Rehema Mercy Makokha, Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili Katika Chuo Kikuu cha Nairobi.Nimekuja kufanya utafiti kuhusu Athari za Sheng’ katika ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili.Kazi hii naifanya kwa ajili ya Kitaalamu. Mchango wa maoni yenu kwangu yatakuwa na manufaa si haba, si tu kwangu bali kwa sekta ya elimu kwa ujumla na maoni yenu yatakuwa siri.Karibu.)

| | |
|---|---|
| Mtafiti (Rehema): | Hujambo? |
| Mtafitiwa (Mwalimu): | Sijambo. |
| Mtafiti (Rehema): | Je, unaonaje matokeo ya mtihani wa Kiswahili mlioufanya? |
| Mtafitiwa (mwalimu) | Sikuridhishwa na matokeo hayo kabisa. |
| Mtafiti (Rehema): | Kwa nini? |
| Mtafitiwa (Mwalimu): | Kwa kuwa wanafunzi hawakupata alama ya kuridhisha,wengi walipata gredi ya C, na C- katika Kiswahili. |
| Mtafiti (Rehema): | Je, wanafunzi wako hutumia Sheng’ katika kuwasiliana? |
| Mtafitiwa (Mwalimu): | Naam, kwa kawaida wakiwa peke yao huwa wanawasiliana kwa kutumia Sheng’. |
| Mtafiti (Rehema): | Kwa maoni yako, je, ni wanafunzi wa kidato kipi ambao wameathirika zaidi? |
| Mtafitiwa (Mwalimu): | Wote wameathirika kwani wanaitumia sana wanapowasiliana haswa nyakati za mapumziko. |
| Mtafiti (Rehema): | Je,walimu na wanafunzi wa shule hii hutumia Sheng’? |

Mtafitiwa (Mwalimu) Naam,wengi wa walimu huwasiliana kutumia hii lugha ya Sheng' wanapokuwa nje ya madarasa hata wafanyikazi hutumia kwa uchache wanapowasiliana haswa wapishi na walinzi .

Mtafiti (Rehema): Na je, mnatumia mbinu gani kuhakikisha kuwa lugha hii haitumiwi shuleni?

Mtahiniwa (Mwalimu): Kwa kweli huwa tunapata wakati mgumu sana kulirekebisha hili ila huwa tunawaadhibu wale wanafunzi wanaopatikana wakiitumia lugha hii kwa kuwapa kazi ya ziada kama vile kufagia au hata kufyeka.

Mtafiti (Rehema): Asante sana mwalimu kwa muda wako na ushirikiano wako. Ninatumai kwamba suala hili litashughulikiwa ili tuweze kuimarisha matokeo ya lugha ya Kiswahili shuleni.

Mtafitiwa (Mwalimu): Karibu sana (tunaagana)

**KIAMBATISHO B: VIELELEZO VYA INSHA**

[redacted] KIDATO CHA KWANZA.

"SIKU YA NYANI KUFA"

Ilikuwa siku ya Jumatatu shuleni mwetu. Wakati huo tulikuwa gwaride, Ghafla bin vuu mpishi aliyepewa jina la lakabu lijulikanalo "Sheshee" alikimbia na kumwita mwalimu aliyezamu. Alimwita kando na kumfahamisha kwa mshtuko. Sisi hatukujua kilichokuwa kikiendelea. Lakini kwa kuangalia sura tuligundua si kitu nzuri. Baadaye Mkuu wa shule alitupasulia na kutwambia ni moto bwenini. Basi ikawa ni kila mwanafunzi kutimua vumbi, kwenda kuzima moto. Hata siku hiyo mamode [walimu] walikimbia.

Kwa uwezo wa Maulana tulizima moto na tukarudi darasani ilikuwa na vipindi [malesions] Msako ukaanza. Kila mwanafunzi kutajwa mshukiwa. Hata wengine kusingiziwa. Vivanja pia kusingiziwa. Lililofikia darasa letu mimi na skide [rafiki wa karibu darasani.] wangu tulitajwa kama washukiwa. Nilijaribu kuwashow [kuwaambia] mamode [walimu] kuwa mimi ni mwenye haki. Lakini hawakutaka kujua.

Bila maelezo mengi wakanituma nyumbani. Basi ikabidi nitoke nje ya shule ili nikaweze kumpigia buda [baba] anitumie bufee [nauli]. Nilipompigia na kumweleza buda [baba] alihiambia kuwa atafika hapo shule baada ya masaa mawili kwa sababu hakuwa nyumbani Btr [Butere] mbali alikuwa hapa kando Kti [Kitui].

Punde si punde gari za abiria zikafika pale stesheni, Zingine zilipita kwa kasi huku madonda [kondakta] wakiwa nje ya milango. Nikijaribu kuangalia magari hayo sauti ngumu ilinishtua. Kumbe alikuwa buda [baba] keshafika. Tunakaingia shuleni pamoja. Tulipofika hadi kwa mwalimu mkuu. Yeye mwenyewe akaeleza kesi yangu. Buda [baba] akauliza makosa yangu.

Alipoambiwa kuwa nimechoma bweni na skide [rafiki ningekaa naye] wangu alishtuka kando macho ya penyeza nje kutoka yalipokuwa. Naye akaniweka sok [ngum] ... [nife]

KIDATO CHA PILI

SIKU SITASAHAU KAMWE

vipindi
Ilikuwa siku moja baada ya Malessons ambapo tulitoka
Marafiki Vizuri
shuleni na Mabeshte wangu Tulikuwa Tumekaa Vinice kiasi
Walimu
ya Kusamba Mamode walitutunza kwa Zawadi tofauti
tofauti.

Tulikuwa tunaendelea kutangatanga kuingia ndani ya hoteli fulani
ili tupate kula. Mara nikasikia mtu kando yangu akitema
Mpenzi msichana mrembo
Bae. Kumtazama alikuwa ni pengting mmoja aliyekuwa
anazungumza na Mpenziwe.

Kikundi cha wanaume pesa
Baada ya Kula Magomaa wangu walitoa ganji na walakalipa
Baada ya kumaliza, niliwambia marafiki mondoke
Alfa Kumado niliwaisho Mabeshte Zangu tujikate. Tulienda
na Tukaabiri gari moja ya matatu ambapo Mabeshte
marafiki pesa nauli manamba
Mabeshte walitoa Ganji Kulipia Bufee kwa yule dondo kwa
Bahati Mbaya pesa hazikuwa zinatosha.

manamba Yungu
Yule Donde alizua Bruhaa na akaamua kutuita polisi.
mipango
fomo zetu ko hazingefaulu kwa kuwa muda si mrefu
Bunduki
walifika polisi na tukaelekezwa Kili. Tukafunga Tulifungwa
Pingu mwanamke deskmate
Kaachta na dumnachia mwingine na kupelekwa ndani. Skide
wangu alikuwa mwoga na kwa sasa tayari alikuwa
analia kwa huzuni.

Baada ya kumaliza
Tulipofikishwa tuliambiwa lazima tulipe faini. Alafu Alfa Kumado
niliwaambia marafiki zangu wanigonje kidogo naja
Niliwaisho mabeshte kwa mine Mazee kiasi tu Nakam.
Mama Pesa pesa
Nilimpigia Masa tenje na akanitumia ganji ambazo
niliwalipa. Deni wa matatu na polisi. Mpaka leo hiyo
Huwa Naikumbuka mara kwa mara.
siku huwanga naikumbuka.

KIDATO CHA TATU.

# SIKU SITAWAHISAHAU.

Ilikuwa saa sita kamili za usiku, nilikuwa na mabeste (marafiki) wa mine (wangu) kwa keja (nyumba). Pia huko ndani ya keja (nyumba) tulikuwa na mapengting (wasichana, warembo). Ilikuwa ni sherehe ya siku ya kuzaliwa ya mine (yangu). Ilikuwa ni dei (siku) ya kusheherekea na mabeste (marafiki).
Nilikuwa na ganji (pesa) kwa hivyo sikuona hasara yoyote kuandaa sherehe hii. Masa (Mama) yangu alikuwa ameenda ambapo nilikuwa pekee yangu kwa keja (nyumba). Pombe kreti nzima ililetwa na pia keki kubwa sana. Ilikuwa nikuparty (nikusheherekea) tu.
Mimi na marafiki wangu tulikunywa na tukabebwa (tukalewa) na pombe. Bash (Sherehe) iliendelea hadi matime (wakati fulani) ambapo jamaa (kijana) alitoa ndeng'a (bunduki) na kutuagiza kila mtu alale chini. Yule muulana alianza kuleta brrcha (matatizo) humo ndani ya nyumba.
Yule jamaa (kijanaa) alianza kutupora (kutuibia) vitu vyetu. Manzi (msichana) mmoja alipigia manjege (makarao) tenje (simu) wakuje. Tulikuwa tumeshtuka tu tulijua mhadhara umetuget (tumepatwa na wasiwasi). Beste (rafiki) yangu mmoja alijaribu kufight (kupigana) nayeye lakini alipigwa soki (ngumi) moja ya kichwa na kufaint (kuzirai).
Yule jamaa (kijana) aliendelea kuleta brrcha (matatizo) lakini punde masanse (mapolisi) wakafika. Wale mapolisi walichukua makidi (mabunduki) na kumfyatua marithe (marisasi) na kummada (kumuua). Pia tulitiwa kacha (pingu) kwa kuwa hatukuwa tunafai kuweka bash (sherehe) matime (wakati) kama hii.

KIDATO CHA NNE

VYOTE VING'AAVYO SI DHAHABU

Ilikuwa alfajiri safi pale katika shule ya upili ya Umoja mixed ila haikuwa safi kwa ghulamu huyu, Kefa. Kefa alikuwa mle kwa majilisi alichapwa kisa kuwa ako na utundu. Baada ya kutoka mle ndani baada ya vita na mamode alichama mdomo wake ~~baada~~ alipomwona pengting aliyeshona umbo la kike. Alimtazama kidemu kile alivyotembea kidogo ajikwae. Kademu hako kalikuwa kanajisajili katika shule hii. Kefa aliingia kwa daro akiwa na tabasamu usoni. Majamaa wake walishindwa kumeeza aje.

Matime kiasi yakasoma, ndipo kademu kaliletwa daro na mode fulani. Alijiongelea na akawa slide wake Kefa. Kefa katika harakati za kumjua aligundua kwa huyu pengting ameomoka, mganji kukuruka. Ila kademu hako alikokuwa akijieleza alitaja kuwa alitoka shule kubwa. Jambo hilo halikuwa akilini mwake Kefa. Malessons na matime yaka songa. Kefa alifaulu kuwa arif wake Karesh. Masaa ya kuendo nyumbani yaliwadia. Dakika chache ndai lenye limekisirika lilidunda. Ilikuwa lao kina Karesh, kweli, ukiona vyaelea ujue vimeundwa.

Siku iliyofuata ilikuwa wikendi, Kefa alivalia mingaro yake aliyoiona nadhifu. Madonda waliletwa brrcha pale kituoni. Shati lake lika chafuka. Kefa alikuwa ameagana na Karesh wapatane. Punde si punde Karesh alidunda na kutembea kwa mwendo unaomfanya tausi apagawe na wivu. Ilikuwa mida ya dumnacha. Kademu hako ~~kilikuwa~~ kiliamua kumtolea form. Wawili hawa waliingia kwa matatu na kulipa bufee ya kufika mta wa KTI. walizunguka huku na kule. Waliingia katika hoteli la kifahari na Karesh akimahidi Kefa kupata vinice. walitoka hapo nakuelekea katika klabu kunywa. Kando ya

lakini Kefa hakuwafuatilia. Waliagiza kinywaji cha chiome [sharubati]. Walipoki wanakunywa. Kefa aliwaona majamaa [waume wengi] wale tena ila hivi sasa walikuwa na marungu

Alifikiri ni kinywaji kinamsumbua ila la! Alipokea saki [ngumi] kuwekwa chini tifla [tambarare]. Aliyempiga alikuwa mpenziwe Karesh fedha. Fedha alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Karesh walipokuwa katika shule ya awali aliyosomea Karesh. Fedha alichukua ndenga [bunduki] na kumfyatulia risasi ya mguu. Alipokea kichapo kidogo kurianya [kufa]. Karesh alimwangalia Kefa huku akicheka. Kefa aliachwa chini akiwa hali mahututi huku akijuta kuwa na urafiki na Karesh kwa kweli majuto ni mjukuu na huja kinyume